Nipashe
Jumatano Juni 22, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580984
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,008,534,842/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#



**Simulizi** ya kusisimua ya afande Mtanzania swahiba mkuu wa Iddi Amin

UKURASA 11



KOCHA MISRI AMSHUTUMU MO SALAH

UKURASA 22



# Kikokotoo mafao bado kaa la moto

HOJA ZA MBUNGE

**Mil. 95/-**
Kiasi ambacho alitakiwa kupata mtumishi mwenye mshahara wa Sh. 1,235,000

**Mil. 47/-**
Kiasi ambacho atapata mtumishi mwenye mshahara wa Sh. 1,235,000

**Tril. 2/-**
Ahadi ya serikali ndani ya Bunge kulipa kiasi hicho kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii 2022/23

**??**
Mbunge Ester Bulaya: Kwa nini hakuna fungu kwa ajili ya malipo ya madeni hayo katika bajeti?

UK. 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 3
**KORTINI SHTAKA KUKUTWA NA NYETI TANO ZA KIKE**
MKAZI wa Maswa, Simiyu mkoani Mwanza, Salum Nkonja maarufu Emmanuel Nkonja,

UKURASA WA 3
UFAFANUZI
**ROTARY CLUB YAIUNGA MKONO EATV KAMPENI YA NAMTHAMINI**
Katika toleo letu la jana tulichapishwa taarifa ya Rotary Club tawi la Oysterbay...

UKURASA WA 4
**TUME YAUNDWA UTATA UHAMISHO WATUMISHI**
WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)...

## Mkurugenzi Jiji Arusha kortini tena kesi ya tatu

UKURASA 5

## Nabii Suguye aongoza maelfu kuliombea Taifa na Rais Samia



Nabii Nicolous Suguye akiongoza maelfu ya waumini katika maombezi maalum ya kuliombea Taifa na Rais Samia Suluhu Hassan kwenye Viwanja vya Sabasaba Mikindani, Mtwara juzi. **Habari Uk.2. PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali, mabalozi wateta kinachoendelea Loliondo

UKURASA 4

**MICHEZO** YANGA NA MKAKATI MZITO CAF UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Kikokotoo mafao bado kaa la moto

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum, Ester Bulaya, amesema ni muhimu serikali ikaweka kikokotoo cha asilimia 50 badala ya asilimia 33 ya sasa ambayo kwa mtazamo wake inampunja mtumishi.

Vilevile, amesema fomula inayopaswa kutumika ni moja ya 480 kwa miaka 12.5 na siyo moja ya 540 kwa miaka 15.5.

Akichangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya serikali kwa mwaka 2022/23, Bulaya alisema fomula hiyo haiwezi kumsaidia mtumishi kwa kuwa anapata mkupuo mdogo, ambao humwezesha kujenga nyumba, kufungua biashara na kusomesha watoto wake.

Mbunge huyo alisema hali iko hivyo kwa kuwa serikali haionyeshi nia ya kulipa madeni ya mifuko ya hifadhi ya jamii, huku akihoji ahadi ya Wizara ya Fedha na Mipango kutenga fedha kwa ajili ya kulipa madeni kwenye bajeti inayopendekezwa kwa mwaka 2022/23.

"Wakati Naibu Waziri wa Fedha na Mipango anajibu swali la Mbunge Halima Mdee kwenye majibu ya msingi, alisema Sh. trilioni mbili zitakuwapo kwenye bajeti hii kulipa deni la mifuko ya hifadhi ya jamii, mbali ya kwamba inalipwa kupitia hati fungani za muda mrefu lakini hii mifuko inahitaji fedha zao zilipwe, lakini hakuna hizo fedha," alisema.

"Kwa sababu hamlipi madeni kwa wakati ndiyo maana mmeleta sheria ya kikokotoo cha kuwaminya watumishi. Siyo sawa, tuliambiwa tusubiri mnakutana na wadau, mmekutana nao na mmeleta asilimia 33 wakati cha mwanzo kabla ya 25 nyie ndiyo mliokibadilisha kutoka asilimia 50.

"Kwanini mnataka muwape asilimia 33 halafu mbaki na fedha yao nyingi? Watumishi ambao wana mishahara midogo, watumishi ambao kama hakuna Rais mwenye huruma wanaweza kukaa miaka mitano bila kuongezwa mishahara, mtumishi ambaye hajajenga, hajaanzisha biashara unamlipa asilimia 33 halafu unasema nyingine utamlipa taratibu na huko kwenye kumlipa umempunguzia mia-ka ya kumlipa baada ya kustaafu."

Alitolea mfano mtumishi wa daraja la TGTS F1 anayepata mshahara wa Sh. 1,235,000 kwa kikokotoo cha asilimia 33 kiinua mgongo chake ni Sh. mil 47, huku akihoji kwa mshahara huo mtumishi wa mshahara mdogo atajenga nyumba saa ngapi na kuanzisha biashara.

Alisema kwa kikokotoo cha moja ya 540 kilichokuwapo mwanzo kwa mshahara huo angestaafu kwa kuchukua asilimia 50 angelipwa Sh. milioni 95 na angebaki na pensheni ya Sh. 500,000 kwa mwezi na angelipwa kwa miaka 15.

"Mnamtengenezea mazingira magumu na bado mnamkadiria afe haraka, hii siyo sawa. Na hawa wafanyakazi ndiyo wanatekeleza hii mipango tunayopitisha hapa," alisema Bulaya.

Wakati mbunge huyo akiendelea kuchangia, Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako, alimpa taarifa kuwa umri wa miaka 12.5 mtumishi atakayeishi zaidi ya miaka hiyo hata 30 ataendelea kulipwa.

Mbunge huyo alikataa kuipokea taarifa hiyo na kuhoji kwanini serikali imeweka miaka 12.5 badala ya 15, akisisitiza kuwa ni kwa sababu serikali imeikopa sana mifuko hiyo na hakuna fedha za kuwalipa wastaafu.

Kwa mujibu wa Bulaya, wadau walitaka fomula ya kikokotoo itumike mishahara minono na serikali ikasema itatumia mishahara bora 10 ndani ya miaka mitatu.

"Watumishi hawa wanaweza kukaa miaka mitano hawajaongezwa mishahara, siyo sawa, wanashindwa kusema kwa sababu mliwabana wawakilishi wa vyama vya wafanyakazi kwenye vikao.

"Ndiyo maana vyama vya wafanyakazi haviwezi kutoka kusema, ninajua hii kanuni siyo msahafu, nendeni mkapitie wapeni asilimia 50 kama hawajajenga wajenge, waanzishe biashara na kusomesha watoto wao," alisema.

Mbunge huyo alisema mifuko itaweza kulipa wastaafu vizuri, ikiwa serikali italipa madeni yake inavyotakiwa.

"Hamuwezi kuwalipa wastaafu wengi kwa sababu mifuko iko hohehahe, mtaweza kulipa ikiwa mtalipa madeni ya mifuko ikawa na uwezo," alishauri.

Baada ya kusema hivyo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, alisimama na kumpa mbunge huyo taarifa kuwa katika mchakato wa kufikia uamuzi ya kikokotoo, siyo kweli kwamba serikali ilivibana vyama vya wafanyakazi visizungumze.

"Wakati wa Mei Mosi, risala ya vyama vya wafanyakazi iliiomba serikali ifanye nini na waliweka wazi mchakato na walikubali ulikuwa shirikishi, namwomba Mbunge Bulaya aende kwenye risala ya vyama vya wafanyakazi kuna kila kitu," alisema.

Hata hivyo, Bulaya alikataa taarifa hiyo na kusema suala la haki ya watumishi lisifanyiwe mchezo na kutaka wapewe asilimia 50, na kwamba ingekuwa haki wangepewa moja ya 480 na siyo moja ya 540.

Mjadala wa kikokotoo uliibuliwa na Nipashe mwaka 2017 baada ya kuchapisha ripoti iliyoonyesha jinsi fomula itakavyokuwa kutokana na kanuni za sheria mpya ya hifadhi ya jamii wakati huo.

Kutokana na jambo hilo kuibua mjadala mkali kitaifa, aliyekuwa Rais wakati huo, Hayati Dk. John Magufuli, alitangaza kuahirishwa kutumika kwa kikokotoo kipya hadi mwaka 2023.

## Nabii Suguye aongoza maelfu kuliombea Taifa na Rais Samia

**Na Mwandishi Wetu,** MTWARA

KIONGOZI wa Kanisa la Huduma ya Neno la Upatanisho (WRM) nchini, Nabii Nicolous Suguye, ameungana na maelfu ya wananchi wa Mkoa wa Mtwara kufanya maombi maalum ya kuliombea Taifa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Maombi hayo yalifanyika katika Viwanja vya Sabasaba vilivyoko Mikindani, Manispaa ya Mtwara juzi ambapo pamoja na mambo mengine, aliongoza kufanyika kwa maombi hayo ya kuliombea Taifa ili Mungu aliweke katika mikono salama hasa wakati huu wenye matatizo lukuki yakiwamo ya magonjwa ya mlipuko kama UVIKO-19.

"Nimekuja Mtwara kwa ajili ya kushirikiana nanyi wananchi kufanya maombi maalum ya kuliombea Taifa letu pamoja na viongozi wetu wakuu katika nchi wakiongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, ambaye sote tunamwombea afya njema na kumkabidhi Mungu katika kulitumikia vyema Taifa letu," alisema.

Nabii Suguye pia alitumia nafasi hiyo kufanya maombi maalum kwa ajili ya Mkoa wa Mtwara na rasilimali zake huku akiwataka wananchi na wakazi wa mkoa huo kumtanguliza Mungu katika shughuli wanazofanya pamoja na kuongeza bidii ya kufanya kazi ili kuleta maendeleo ya mtu mmoja mmoja, mkoa na taifa kwa ujumla.

"Ndugu zangu, nimewaombea baraka kwa Mungu lakini niwaombe sana mwongeze juhudi katika kufanya kazi, ninajua wananchi wa mkoa huu ni wachapaka kazi sana lakini ni wajibu wangu kama kiongozi wa dini kuwakumbusha kuwa hakuna sababu ya kulala zaidi ya kuamka na kufanya kazi kwa bidii na maarifa," alisema.

Nabii Suguye pia alisema ni jambo la kuendelea kumshukuru Mungu kuona nchi imeendelea kuwa salama na watu wake wamekuwa na umoja na mshikamano lakini hiyo haina maana ya kutofanya maombi na ndiyo maana ameamua kufika kwenye mkoa huo na kumwomba Mungu kwa pamoja ili kufanikisha neema na baraka iliyopo katika mikoa ya kusini iwanufaishe wananchi wote.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE — BBN Limited TZA

**REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST FOR THE PROVISION OF Tubular Steel Piles**

**REF : ETJ-BB-PR-EI-GEN-FO-0001-00.**

BESIX Ballast Nedam Limited, the CONTRACTOR for the Engineering, procurement and Construction of the Jetty and Load Out Facilities in the Tanga Bay for the East African Crude Oil Pipeline (EACOP) Project, invites experienced specialist Companies to express their interest for:

**Fabrication, Supply and Delivery of coated Tubular Steel Piles.**

The Republic of Uganda, the Uganda National Oil Company (UNOC), the United Republic of Tanzania and/or Tanzania Petroleum Development Corporation (TPDC), as well as other international oil companies are partaking in the implementation of the EACOP Project.

As part of EACOP project, the Crude oil will be loaded on vessels via a facility located in the near shore environment of the Indian Ocean. The Facility will be located 2 km offshore from the Marine Storage Terminal site located on the Chongoleani peninsula in front of Tanga Port in Tanzania.

**BRIEF DESCRIPTION OF THE SCOPE OF THE MATERIALS / SERVICES:**
- Spirally welded Tubular Steel Piles,
- Different length of piles up to 82.28m,
- Diameter of the piles: 1,168mm; 1,219mm or 1,524mm,
- Thickness of the piles: 18mm; 19mm; 20mm; 22mm; 24mm,
- A topper part of each pile is coated,
- On each pile there are lifting holes, pile marking and depth marking,
- Shear keys are installed on some piles,
- Transport FOB incoterms Liner out,
- Total steel 7,412 tons, and 9,586m$^2$ of coating;

**MINIMUM REQUIREMENTS:**
Companies expressing their interest are invited to document their request with :
- Qualified workers and certified QA/QC ;
- EXC4 certified
- Inspectors to be Level III certified ;
- Operators to be certified acc to ACQPA/Frosio ;
- Ability for Steel dressing full P3 as per ISO 12944, for Grade of Cleanliness Sa 3 as per ISO 8501 ;
- Fabrication at fabrication yard, not on site ;
- Warranty of 5 years for rusting Ri2, and Cracking, Blistering, Flaking Q3S3 ;
- Coating from Carboline, Hempel, Jotun or PPG ;
- Company profile with prove of sufficient financial capabilities and sufficient and capable resources.
- An experience list with relevant supply history / track record showing minimum of five (5) years' experience in execution similar services of required fabrication and transport as per international standards common in the Oil and Gas business or comparable market,
- CE marked as per CPR and BS EN 1090 ;
- Manufacturing requirements API 5L or EN 10219.
- Company's Quality and HSE plans and certification: ISO 9001:2015, ISO 14001:2015, OHSAS 18001 (ISO45001:2018), EN ISO 14732, EN ISO 90606-1, ISO 11484, EN ISO 90609-1, EN ISO 10893-8, 10893-11, or equivalent certificates;
- Compliance with petroleum (local Content) regulation of 2017 and local company definition for Tanzania.
- Proof of registration/application to Local Supplier Service Provider (LSSP) database at the time of submission of the response to this expression of interest is highly recommended.

Interested companies which meet the minimum requirements and have the capacity to provide the services listed above should express their interest by sending together with the above listed documents an email to **procurement@bbnjv.com (Max. Email Size: 20 MBs & All documents must be submitted in the English language)** on or before **6th of July 2022, 12 noon Tanzania Time,**

Companies satisfactorily meeting the above minimum requirements will be evaluated and if selected will be invited, subject to the signature of a Non-Disclosure Agreement (NDA), to participate in the bidding process.

**Note:** Only pre-qualified companies will receive an invitation to submit their bid in furtherance of the Call for Tender process.

216913201

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE — BBN Limited TZA

**REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST FOR THE PROVISION OF ENGINEERING, FABRICATION, SUPPLY of Launching Girder and Feeding Trolley**

**REF ETJ-BB-PR-EI-GEN-LG-0001-00**

BESIX Ballast Nedam Limited, the CONTRCATOR for the Engineering, procurement and Construction of the Jetty and Load Out Facilities in the Tanga Bay for the East African Crude Oil Pipeline (EACOP) Project, invites experienced specialist Companies to express their interest for :

Engineering, Fabrication, and Supply of a Launching Girder and a Feeding Trolley.

The Republic of Uganda, the Uganda National Oil Company (UNOC), the United Republic of Tanzania and/or Tanzania Petroleum Development Corporation (TPDC), as well as other international oil companies are partaking in the implementation of the EACOP Project.

As part of EACOP project, the Crude oil will be loaded on vessels via a facility located in the near shore environment of the Indian Ocean. The Facility will be located approximately 2 km offshore from the Marine Storage Terminal site located on the Chongoleani peninsula in front of Tanga Port in Tanzania.

**BRIEF DESCRIPTION OF THE SCOPE :**

Part of the Jetty shall be constructed with a special self-launching piling equipment (Launching Girder) fitted with a Hammer stand, and a Feeding Trolley.

**The Launching Girder will enable to :**
- Manipulate, position and drive, within tolerances, piles 1168mm wide and 32.25m long,
- Manipulate, position within tolerances and install crossheads, truss elements of the trestle,
- Cutting, welding, sandblasting and painting,
- Progress with from previous bent to new bent,
- Store office, sanitary and storage containers.

**A Trolley that will allow to:**
- supply the launching girder of all material and consumable required for the construction activities above mentioned.

A Hammer Stand that can hold Piling hammer, power packs and reel for hammer hoses.

**MINIMUM REQUIREMENTS:**
Equipment shall be delivered as following :
- Design of equipment in 4 months (M1-M4),
- Procurement and fabrication of equipment in 6 months (M1-M6),
- Pre-assembly and testing at yard Month 6,
- Assembly and commissioning on site Month 9,
- Able to withstand 38 tons of live loads,
- Able to withstand continuous power of 60kW for 11 equipment,
- 24 months warranty.

Companies expressing their interest are invited to document their request with
- Company profile with prove of sufficient financial capabilities and sufficient and capable resources.
- An experience list with relevant supply history / track record showing minimum of five (5) years' experience in execution similar services of required Engineering, fabrication and supply as per international standards common in the Oil and Gas business or comparable market,
- Company's Quality and HSE plans and certification: ISO 9001:2015, ISO 14001:2015, OHSAS 18001 (ISO45001:2018), EN ISO 14732, EN ISO 90606-1, ISO 11484, EN ISO 90609-1, EN ISO 10893-8, 10893-11, or equivalent certificates;
- CE marked as per CPR and BS EN 1090 ;
- Compliance with petroleum (local Content) regulation of 2017 and local company definition for Tanzania.
- Proof of registration/application to Local Supplier Service Provider (LSSP) database at the time of submission of the response to this expression of interest is highly recommended.

Interested companies which meet the minimum requirements and have the capacity to provide the services listed above should express their interest by sending together with the above listed documents an email to **procurement@bbnjv.com (Max. Email Size: 20 MBs & All documents must be submitted in the English language)** on or before **6th of July 2022, 12 noon Tanzania Time,**

Companies satisfactorily meeting the above minimum requirements will be evaluated and if selected will be invited, subject to the signature of a Non-Disclosure Agreement (NDA), to participate in the bidding process.

**Note**: Only pre-qualified companies will receive an invitation to submit their bid in furtherance of the Call for Tender process.

216913201

# UFAFANUZI

## Rotary Club yaiunga mkono EATV kampeni Namthamini

Katika toleo letu la jana tulichapishwa taarifa ya Rotary Club tawi la Oysterbay kukabidhi pedi 10,500 katika kituo cha East Afrika Televisheni na Radio ikiwa ni ushirikiano wa kampeni ya 'Namthamini' inayolenga kugawa pedi kwa wanafunzi ili kuwasaidia kuwa salama wanapokuwa kwenye hedhi.

Hata hivyo, jina la klabu hiyo lilikosewa na kuandikwa Lottery. Tuomba radhi kwa usumbufu wowote uliojitokeza.

Taarifa hiyo kamili ilisema katika hafla ya kukabidhi taulo hizo, Rais wa klabu hiyo, Aisha sykes, alisema wameguswa kushiriki kampeni hiyo ili kumaliza changamoto ya watoto wa kike kutohudhuria masomo kwa sababu ya kupata hedhi.

Alisema mchango huo ni takwa la klabu za Rotary kote ulimwenguni la kushirikiana na serikali na mashirika yanayofanya kazi ya kusaidia jamii ili kuziwezesha katika juhudi zao.

"Nikiwa kama mwakilishi wa kampeni klabu ya Rotary kimataifa ya kumwezesha msichana nilivutiwa na kampeni ya Namthamini kwa kuwa ina lengo ya kumsaidia mtoto wa kike kuendelea na masomo," alisema Aisha.

Alisema kupitia programu yao ya kuwapa ufadhili wa masomo ya elimu ya juu mabinti wa kitanzania tangu mwaka 2010, wamegundua kuwa wasichana wengi hawamalizi masomo ya sekondari kutokana na kukosa taulo za kujisitiri wanapopata hedhi.

"Wasichana wengi hawana uwezo wa kuomba ufadhili huu wa kwa sababu hawamalizi elimu ya sekondari. Na hawamalizi elimu ya sekondari kwa sababu wanakumbana na changamoto ya kutafuta taulo za kike kila mwezi," alisema.

Alisema kuwa licha ya kukabidhi msaada huo bado wanaendelea kukusanya michango kwenye matawi mengine ili wachangie pedi zitakazowezesha wasichana 1,200 kuhudhuria masomo mwaka mzima.

Mwenyekiti wa Kampuni ya IPP, Abdiel Mengi, aliishukuru klabu hiyo kwa kushirikiana nayo kufanikisha kampeni ya Namthamini iliyolenga kuhakikisha kuwa hedhi haiwi kikwazo cha mabinti kukosa masomo.

Alisema kampeni hiyo ni moja ya programu za kumnyanyua mwanamke zinazofanywa na kampuni ikiwa ni shauku ya muda mrefu ya kurudisha fadhila kwa jamii.

Meneja Uhusiano wa Wateja wa EATV/Radio ambaye ni Meneja wa mradi huo, Nancy Mwanyika, aliishukuru klabu hiyo kwa kuwapatia misaada hiyo na kusema kuwa mchango huo utaweka shule jumla ya wasichana 800 mwaka mzima.

"Kwa niaba ya East Africa Television na Radio tunapenda kuwashukuru klabu ya Rotary kwa msaada tulioupokea leo na mingine waliotuahidi kutoa," alisema Nancy.

Alisema katika kampeni hiyo wanashirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na mwaka huu wanatarajia kuwafikia wasichana walipo kwenye mikoa ya Mtwara, Njombe na Ruvuma.

# Kortini shtaka la kukutwa na nyeti tano za kike

**Na Grace Gurisha**

MKAZI wa Maswa, Simiyu mkoani Mwanza, Salum Nkonja maarufu Emmanuel Nkonja, amependishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu akikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi yenye mashtaka 11 likiwamo la kukutwa na sehemu za siri tano za kike na chuchu tano za wanawake.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali, Carolina Matemu, alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Ramadhani Rugemalira kuwa mshtakiwa alikutwa pia na nyara za serikali, yakiwamo mafuvu mawili ya binadamu na sehemu za siri za wanyama.

Matemu alidai Oktoba 30, 2017, wilayani Ubungo, jijini Dar es Salaam, mshtakiwa huyo alikutwa na sikio na pembe ya nyati vyote vikiwa na thamani ya Sh. 4,318,700 bila kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori.

Alidai kuwa, katika tarehe na eneo hilo, mshtakiwa huyo pia alikutwa na uume wa mbwamwitu wenye thamani ya Sh. 2,272,600, pamoja na uume wa nyumbu wenye thamani ya Sh. 1,477,450 bila kibali.

Ilidaiwa kuwa, Novemba 30, 2017, Wilaya ya Ubungo, Dar es Salaam, mshtakiwa huyo alikutwa na mikia mitano ya ngiri yenye thamani ya Sh. 5,114,250, uume wa fisi mitatu, yenye thamani ya Sh. 3,750,450.

Pia, mshtakiwa alikutwa akimiliki yai moja la mbuni lenye thamani ya Sh. 2,827,600, ngozi moja iliyokaushwa ndege aina ya Ngekewa yenye thamani ya Sh. 227,300 na kichwa kimoja cha nyoka aina ya Kobla chenye thamani ya Sh. 193,205.

Pia mshtakiwa huyo alikutwa akimiliki viungo vya binadamu ambavyo ni sehemu za siri tano za wanawake, mafuvu mawili ya binadamu na chuchu tano za wanawake.

Mshtakiwa alikana mashtaka hayo na upande wa mashtaka ulidai, upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba tarehe nyingine ya kumsomea mshtakiwa hoja za awali.

Hakimu alimweleza mshtakiwa atakuwa nje kwa dhamana ikiwa atatimiza sharti la kuwa na wadhamini wawili watakaosaini bondi ya Shilingi milioni tano.

Hakimu aliahirisha kesi hiyo hadi Julai 5, 2022 na mshtakiwa alipelekwa mahabusu kwa kukosa wadhamini.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
June 21, 2022

# TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Ijumaa Tarehe **28/06/2022** kampuni ya **EFFCO SOLUTION LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **MPAKA WA HOLILI** kuelekea **MOSHI MJINI – KIWANDA CHA SERENGETI BREWERIES**, Magari hayo yenye namba za usajili:

**1. KCR725T / ZE2560**
Gari linavipimo vifuatavyo
**Urefu - mita 21.99**
**Upana - mita 5.75**
**Kimo - mita5.30**

**2. KCR330V /ZG0790**
Gari linavipimo vifuatavyo
**Urefu- mita 21.99**
**Upana - mita 3.50**
**Kimo - mita 5.30**

**3. KCR720T /ZC8804**
Gari linavipimo vifuatavyo
**Urefu - mita 21.99**
**Upana - mita 4.00**
**Kimo - mita 5.30**

**4. KCW052Z /ZG3212**
Gari linavipimo vifuatavyo
**Urefu - mita 30.00**
**Upana - mita 5.75**
**Kimo - mita 5.30**

**5. KCR724T /ZD1873**
Gari linavipimo vifuatavyo
**Urefu - mita 21.99**
**Upana - mita 4.80**
**Kimo - mita 5.30**

**6. KCR331V /ZG0789**
Gari linavipimo vifuatavyo
**Urefu - mita 21.99**
**Upana - mita 5.75**
**Kimo - mita 5.30**

**7. KCR719T /Z9537**
Gari linavipimo vifuatavyo
**Urefu - mita 30.00**
**Upana - mita 5.75**
**Kimo - mita 5.30**

3. Njia itakayotumika **MPAKA WA HOLILI** mpaka **MOSHI MJINI – KIWANDA CHA SERENGETI BREWERIES** gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE — BBN Limited TZA

**REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST FOR THE PROVISION OF Fabrication, Supply and Delivery of Structural Steel Trusses, Crude Oil Pipes, GRE pipes, Cable Ladders, HDG Gratings, Catwalks and Crossheads**

**REF : ETJ-BB-PR-EI-GEN-SF-0001-00.**

BESIX Ballast Nedam Limited, the CONTRACTOR for the Engineering, procurement and Construction of the Jetty and Load Out Facilities in the Tanga Bay for the East African Crude Oil Pipeline (EACOP) Project, invites experienced specialist Companies to express their interest for:

Fabrication, Supply and Delivery of coated Structural Steel Trusses, Crude Oil Pipes, GRE pipes, Cable Ladders, HDG Gratings, Catwalks and Coated Crossheads.

The Republic of Uganda, the Uganda National Oil Company (UNOC), the United Republic of Tanzania and/or Tanzania Petroleum Development Corporation (TPDC), as well as other international oil companies are partaking in the implementation of the EACOP Project.

As part of EACOP project, the Crude oil will be loaded on vessels via a facility located in the near shore environment of the Indian Ocean. The Facility will be located 2 km offshore from the Marine Storage Terminal site located on the Chongoleani peninsula in front of Tanga Port in Tanzania.

**BRIEF DESCRIPTION OF THE SCOPE OF THE MATERIALS / SERVICES:**
- Steel Truss Units of 12, 24 and 48m long, 3.60 to 5.60m wide and 5m height, complete with main pipe 30 inch pipe inside on pipe supports, guardrails included,
- Steel bracings for loops' structures,
- Steel Crosshead as support for trusses,
- Steel Catwalks between dolphins,
- Steel Mezzanine on LOF,
- All the above is coated,
- Cable Ladders for the full jetty length,
- HDG Gratings for road and pedestrian access
- Transport FOB incoterms Liner out
- Total steel 2,832 tons, and 7000 M2 of coating.

**MINIMUM REQUIREMENTS:**
Companies expressing their interest are invited to document their request with:
- Qualified workers and certified QA/QC;
- Inspectors to be Level III certified;
- Operators to be certified acc to ACQPA/Frosio;
- Ability for Steel dressing full P3 as per ISO 12944, for Grade of Cleanliness Sa 3 as per ISO 8501;
- Fabrication at fabrication yard, not on site ;
- Warranty of 5 years for rusting Ri2, and Cracking, Blistering, Flaking Q3S3;
- Coating from Carboline, Hempel, Jotun or PPG;
- Company profile with prove of sufficient financial capabilities and sufficient and capable resources.
- An experience list with relevant supply history / track record showing minimum of five (5) years' experience in execution similar services of required fabrication and transport as per international standards common in the Oil and Gas business or comparable market,
- CE marked as per CPR and BS EN 1090;
- Company's Quality and HSE plans and certification : ISO 9001:2015, ISO 14001:2015, OHSAS 18001 (ISO45001:2018), EN ISO 14732, EN ISO 90606-1, ISO 11484, EN ISO 90609-1, EN ISO 10893-8, 10893-11, or equivalent certificates;
- Compliance with petroleum (local Content) regulation of 2017 and local company definition for Tanzania.
- Proof of registration/application to Local Supplier Service Provider (LSSP) database at the time of submission of the response to this expression of interest is highly recommended.

Interested companies which meet the minimum requirements and have the capacity to provide the services listed above should express their interest by sending together with the above listed documents an email to **procurement@bbnjv.com (Max. Email Size: 20 MBs & All documents must be submitted in the English language)** on or before **6th of July 2022, 12 noon Tanzania Time,**

Companies satisfactorily meeting the above minimum requirements will be evaluated and if selected will be invited, subject to the signature of a Non-Disclosure Agreement (NDA), to participate in the bidding process.

**Note:** Only pre-qualified companies will receive an invitation to submit their bid in furtherance of the Call for Tender process.

216913201



EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE — BBN Limited TZA

**REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST FOR THE PROVISION OF Sacrificial Anodes Cathodic Protection**

**REF : ETJ-BB-PR-EI-GEN-EF-0001-00.**

BESIX Ballast Nedam Limited, the CONTRACTOR for the Engineering, procurement and Construction of the Jetty and Load Out Facilities in the Tanga Bay for the East African Crude Oil Pipeline (EACOP) Project, invites experienced specialist Companies to express their interest for:

**Fabrication, Supply and Delivery of Sacrificial Anodes Cathodic Protection (SACP).**

The Republic of Uganda, the Uganda National Oil Company (UNOC), the United Republic of Tanzania and/or Tanzania Petroleum Development Corporation (TPDC), as well as other international oil companies are partaking in the implementation of the EACOP Project.

As part of EACOP project, the Crude oil will be loaded on vessels via a facility located in the near shore environment of the Indian Ocean. The Facility will be located 2 km offshore from the Marine Storage Terminal site located on the Chongoleani peninsula in front of Tanga Port in Tanzania.

**BRIEF DESCRIPTION OF THE SCOPE OF THE MATERIALS / SERVICES:**
- Sacrificial anodes for permanently immersed Jetty piles,
- Design and supply of clamp assemblies,
- Clamps assemblies are coated,
- Transport FOB incoterms Liner out

**MINIMUM REQUIREMENTS:**
Companies expressing their interest are invited to document their request with:
- Qualified workers and certified QA/QC;
- Ability for Steel dressing full P3 as per ISO 12944, for Grade of Cleanliness Sa 3 as per ISO 8501;
- Fabrication at fabrication yard, not on site;
- Design life of 25 years with no maintenance in first 15 years.
- Coating from Carboline, Hempel, Jotun or PPG;
- Company profile with prove of sufficient financial capabilities and sufficient and capable resources.
- An experience list with relevant supply history / track record showing minimum of five (5) years' experience in execution similar services of required fabrication and transport as per international standards common in the Oil and Gas business or comparable market,
- Design standards: DNV RP B401;
- Company's Quality and HSE plans and certification: ISO 9001:2015, ISO 14001:2015, OHSAS 18001 (ISO45001:2018) or equivalent certificates;
- CE marked as per CPR and BS EN 1090;
- Compliance with petroleum (local Content) regulation of 2017 and local company definition for Tanzania.
- Proof of registration/application to Local Supplier Service Provider (LSSP) database at the time of submission of the response to this expression of interest is highly recommended.

Interested companies which meet the minimum requirements and have the capacity to provide the services listed above should express their interest by sending together with the above listed documents an email to **procurement@bbnjv.com (Max. Email Size: 20 MBs & All documents must be submitted in the English language)** on or before **6th of July 2022, 12 noon Tanzania Time.**

Companies satisfactorily meeting the above minimum requirements will be evaluated and if selected will be invited, subject to the signature of a Non-Disclosure Agreement (NDA), to participate in the bidding process.

**Note:** Only pre-qualified companies will receive an invitation to submit their bid in furtherance of the Call for Tender process.

216913201

# Serikali, mabalozi wateta kuhusu sakata la Loliondo

**Na Halfani Chusi**

SERIKALI imekutana na mabalozi mbalimbali wanaoziwakilisha nchi zao nchini pamoja na wawakilishi wa mashirika ya kimataifa kujadili mustakabali wa kinachoendelea Loliondo na Ngorongoro.

Jijini Dar es Salam jana, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, alipokutana na wadau hao katika kikao hicho maalum, alikanusha uvumi ulioenea ukidai serikali imetumia nguvu na kukiuka haki za binadamu katika kuwahamisha baadhi ya wakazi walioko maeneo hayo.

Alisema taarifa hizo siyo za kweli na zinapaswa kupuuzwa huku akibainisha kuwa serikali imetenga maeneo maalum kwa ajili yao na mtu atahamia kwa hiari yake mwenyewe kutokana na kuvutiwa na huduma zilizowekwa na serikali.

Balozi Mulamula alisema kikao hicho kilikuwa mahususi kwa kutoa sintofahamu kwa baadhi ya mabalozi, wadau wa mashirika ya kitaifa na wananchi wengine kuhusu kinachotajwa kuwa mgogoro kuhusu Loliondo na Ngorongoro.

"Katika vikao vyetu hivi vya kupashana habari, tumekuwa pia tukiwaalika mawaziri wa sekta hizo. Kumekuwa na taarifa mbalimbali zikisambaa zikidai Loliondo na Ngorongoro wananchi wanaondolewa kwa nguvu na kwa kukiuka haki za binadamu.

"Kwa hiyo, leo ninadhani ufafanuzi uliotolewa na Naibu Waziri (Mary Masanja) pamoja na Mkurugenzi wa Wanyamapori katika wasilisho hili limeondoa sintofahamu kwenye vichwa vya watu," alisema.

Kwa hiyo kinachoendelea Loliondo siyo kuhamisha watu kwamba sasa kumewekwa mipaka upande mmoja kwa ajili ya wanyama na uhifadhi lakini eneo lingine ni kwa ajili ya wananchi na zaidi Km 2,500 zimeachwa kwa ajili yao.

"Kwa hiyo, hakuna anayeondolewa, wanaoondoka ni wa kutoka Ngorongoro kwa sababu kule watu wamepoteza watoto wao, watu wanaliwa na wanyama wakali.

"Kwa hiyo, serikali baada ya kuliona hilo, imekuja na mkakati kabambe wa kuwatafutia maeneo mengine na kuwapatia mazingira mazuri yenye huduma nyingi za kijamii na wamepewa zaidi ya ekari tano kwa wote wanaohamia Loliondo na baadhi ya wakazi zaidi ya 200 wameshaanza kuhamia huko," alifafanua.

Alisema kuwa hali iko shwari licha ya askari mmoja kuuawa wakati wa kutetea amani lakini hakuna anayelisemea hilo, akibainisha kuwa taarifa ya serikali imepokewa kwa furaha na mabalozi kutokana na kuwa na ufafanuzi mzuri.

"Hakuna anayeshurutishwa kuondoka, hakuna anayeondolewa kwa nguvu. Wanaondoka kwa hiari lakini wakiona faida kule, wanakohamia kuna huduma nzuri wataenda wenyewe.

"Kwa hiyo, sisi kama wizara tumetaka jumuiya ya kimataifa, mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao pamoja na wananchi wengine, waelewe kwa ufasaha zaidi kile kinachoendelea dhidi ya sakata hilo," alisisitiza.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, alisema kumakuwapo na uvunjifu wa sheria kwa baadhi ya wakazi wanaoishi maeneo hayo, hali iliyopelekea serikali kuwatafutia njia nyingine ya kuishi.

Alisema sheria iliyowekwa kwa wananchi wanaishi Ngorongoro haimruhusu mkazi kufanya shughuli nyingine za kujamii zaidi ya kufuga tu.

"Ni kula tu, tukasema hapana, sasa tuwaelimishe hawa watu kama unataka kufanya biashara, kama unataka kuendesha pikipiki, kujenga ghorofa, tutoe eneo maalum ambalo litakuwa hiari mtu kutoka katika maisha hayo kwenda katika maisha mengine kwa sababu kama binadamu anapaswa kuishi vizuri.

"Kwa hiyo, tukasema kwetu sisi kama kweli Watanzania tunaangalia haki za binadamu, kuna haja ya kuwasaidia hawa watu kwa sababu wengine wanateseka na wengine wapo katika hatari ya kuliwa na wanyama wakali kama vile simba," alisema.

Mmoja wa wakazi wa Ngorongoro, Jumanne Jafari, alipiga simu katika mkutano huo wa jana na kukiri kuwapo kwa hatua hizo na baadhi ya watu wameanza kuhama Loliondo na wengine wanajiandaa kuhamia kwenye makazi mapya yaliyoandaliwa na serikali mkoani Tanga.

# Tume yaundwa utata uhamisho watumishi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA



WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, amesema tume imeundwa kuchunguza kuhamishwa kwa watumishi 12 mkoani Tanga ambao walighushi nyaraka za uhamisho.

Vilevile, kutokana na kuwapo kwa vitendo hivyo vya kughushi nyaraka za uhamisho, waziri huyo amemwelekeza Katibu Mkuu, Prof. Riziki Shemdoe, kuwa mtu pekee anayetia saini barua za uhamisho.

Bashungwa alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na watumishi wa ofisi hiyo ikiwa ni maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma ambayo huadhimishwa Juni 16 hadi 23 kila mwaka.

"Kuna mambo ya kimjini mjini nadhani mtakuwa mmeyasikia, watumishi zaidi ya 12 ndani ya miezi michache wamehamishwa kwa barua zilizosainiwa kwa niaba ya Katibu Mkuu wakati Katibu Mkuu hajui," alisema.

Waziri huyo alisema tabia hiyo inasababisha serikali kutumia fedha nyingi kuwahamisha watumishi ambao hawajafuata utaratibu.

"Kwa hili sitaki kusikia kuna mtumishi anahusika na timu imeundwa kuchunguza jambo hili," alisema.

Aliwataka watumishi hao kutoshiriki kwenye vitendo vya ovyo ikiwamo kughushi barua za uhamisho wa watumishi.

"Tunakwenda kulisimamia kikamilifu ili kuwe na uwiano sawa wa ikama kwa mijini na vijijini na hili kuanzia sasa lisimamiwe na Katibu Mkuu mwenyewe," aliagiza.

Kuhusu utunzaji siri, Waziri Bashungwa alisema suala hilo kwa watumishi wa wizara yake si hiyari, bali ni lazima na kuwataka kujiepusha na vitendo vya rushwa.

"Watumishi wa Ofisi ya Rais-TAMISEMI wana wajibu wa kutunza siri za serikali kama maelekezo ya viongozi wa juu na hasa ikizingatiwa kuwa asilimia 70 ya watumishi wa umma wanatoka TAMISEMI," aliagiza.

Pia alimtaka Katibu Mkuu kuhakikisha watumishi wanatekeleza wajibu wao ambao unakwenda sambamba na kupewa haki zao.

Katibu Mkuu, Prof. Shemdoe, aliahidi kutekeleza maelekezo ya waziri huyo na kuwataka watumishi hao kuwa waadilifu.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE — BBN Limited TZA

## REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST FOR THE PROVISION OF Fenders and Bollards.

**REF : ETJ-BB-PR-EI-JPT-EF-0001-00.**

BESIX Ballast Nedam Limited, the CONTRACTOR for the Engineering, procurement and Construction of the Jetty and Load Out Facilities in the Tanga Bay for the East African Crude Oil Pipeline (EACOP) Project, invites experienced specialist Companies to express their interest for:

Design, Fabrication, Testing, Supply, Delivery and on-site inspection of fenders and bollards.

The Republic of Uganda, the Uganda National Oil Company (UNOC), the United Republic of Tanzania and/or Tanzania Petroleum Development Corporation (TPDC), as well as other international oil companies are partaking in the implementation of the EACOP Project.

As part of EACOP project, the Crude oil will be loaded on vessels via a facility located in the near shore environment of the Indian Ocean. The Facility will be located 2 km offshore from the Marine Storage Terminal site located on the Chongoleani peninsula in front of Tanga Port in Tanzania.

**BRIEF DESCRIPTION OF THE SCOPE OF THE MATERIALS / SERVICES:**

- Two fenders on the dolphin's for tankers and three fenders on the Platform for barges,
- Each fender contain a rubber cone, a front panel, chains and fixings for front panel-rubber,
- Four T-shape bollards placed on the platform,
- Cast-in inserts for each fender and each bollard,
- Front panel of the fenders and bollards are coated,
- Transport FOB incoterms Liner out;

**MINIMUM REQUIREMENTS:**

Companies expressing their interest are invited to document their request with :

- Qualified workers and certified QA/QC ;
- Quality Control Agency witnessing the tests: BV, DNV-GL or ABS;
- Ability for Steel dressing full P3 as per ISO 8501, for Grade of Cleanliness Sa 3 as per ISO 8501 ;
- Fabrication at fabrication yard, not on site ;
- Warranty period of 24 months and 5 years on latent defects after expiry of the warranty period;
- Coating from Carboline, Hempel, Jotun or PPG ;
- Company profile with prove of sufficient financial capabilities and sufficient and capable resources.
- An experience list with relevant supply history / track record showing minimum of five (5) years' experience in execution similar services of required fabrication and transport as per international standards common in the Oil and Gas business or comparable market,
- Design standards: BS 6349-4 (2014) or PIANC WG33;
- Company's Quality and HSE plans and certification : ISO 9001:2015, ISO 14001:2015, OHSAS 18001 (ISO45001:2018) or equivalent certificates ;
- CE marked as per CPR and BS EN 1090 ;
- Compliance with petroleum (local Content) regulation of 2017 and local company definition for Tanzania.
- Proof of registration/application to Local Supplier Service Provider (LSSP) database at the time of submission of the response to this expression of interest is highly recommended.

Interested companies which meet the minimum requirements and have the capacity to provide the services listed above should express their interest by sending together with the above listed documents an email to **procurement@bbnjv.com** **(Max. Email Size: 20 MBs & All documents must be submitted in the English language)** on or before **6th of July 2022, 12 noon Tanzania Time,**

Companies satisfactorily meeting the above minimum requirements will be evaluated and if selected will be invited, subject to the signature of a Non-Disclosure Agreement (NDA), to participate in the bidding process.

**Note:** Only pre-qualified companies will receive an invitation to submit their bid in furtherance of the Call for Tender process.

216913201



EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE — BBN Limited TZA

## REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST FOR THE PROVISION OF Gangway Tower

**REF : ETJ-BB-PR-EI-JPT-EF-0002-00.**

BESIX Ballast Nedam Limited, the CONTRACTOR for the Engineering, procurement and Construction of the Jetty and Load Out Facilities in the Tanga Bay for the East African Crude Oil Pipeline (EACOP) Project, invites experienced specialist Companies to express their interest for:

Design, Fabrication, Supply, Delivery and Installation Supervision of Gangway Tower.

The Republic of Uganda, the Uganda National Oil Company (UNOC), the United Republic of Tanzania and/or Tanzania Petroleum Development Corporation (TPDC), as well as other international oil companies are partaking in the implementation of the EACOP Project.

As part of EACOP project, the Crude oil will be loaded on vessels via a facility located in the near shore environment of the Indian Ocean. The Facility will be located 2 km offshore from the Marine Storage Terminal site located on the Chongoleani peninsula in front of Tanga Port in Tanzania.

**BRIEF DESCRIPTION OF THE SCOPE OF THE MATERIALS / SERVICES:**

- Column anchored Gangway Tower with self-levelling steps,
- Hydraulic crane incl. control station and remote pendant,
- All mechanical and electrical items of the Gangway Tower (alarm, lighting,...),
- Cast-in inserts of the Gangway Tower with the anchor template,
- Access between Mezzanine and Gangway Tower,
- All the above are protected against corrosion (coating or HDG),
- Transport FOB incoterms Liner out;

**MINIMUM REQUIREMENTS:**

Companies expressing their interest are invited to document their request with :

- Qualified workers and certified QA/QC ;
- Quality Control plan: organisation and responsibilities, inspection and test plan, notification of inspection, non-conformance control, manufacturers data record and inspection release certificates;
- Ability for Steel dressing full P3 as per ISO 12944, for Grade of Cleanliness Sa 3 as per ISO 8501 ;
- Fabrication at fabrication yard, not on site ;
- Coating from Carboline, Hempel, Jotun or PPG ;
- Company profile with prove of sufficient financial capabilities and sufficient and capable resources.
- An experience list with relevant supply history / track record showing minimum of five (5) years' experience in execution similar services of required fabrication and transport as per international standards common in the Oil and Gas business or comparable market,
- Standards: BS 6349 (Maritime Works);
- Welding standard: BS EN 1011;
- Company's Quality and HSE plans and certification : ISO 9001:2015, ISO 14001:2015, OHSAS 18001 (ISO45001:2018);
- CE marked as per CPR and BS EN 1090 ;
- Compliance with petroleum (local Content) regulation of 2017 and local company definition for Tanzania.
- Proof of registration/application to Local Supplier Service Provider (LSSP) database at the time of submission of the response to this expression of interest is highly recommended.

Interested companies which meet the minimum requirements and have the capacity to provide the services listed above should express their interest by sending together with the above listed documents an email to **procurement@bbnjv.com** **(Max. Email Size: 20 MBs & All documents must be submitted in the English language)** on or before **6th of July 2022, 12 noon Tanzania Time,**

Companies satisfactorily meeting the above minimum requirements will be evaluated and if selected will be invited, subject to the signature of a Non-Disclosure Agreement (NDA), to participate in the bidding process.

**Note:** Only pre-qualified companies will receive an invitation to submit their bid in furtherance of the Call for Tender process.

216913201

HABARI KITAIFA

## Wizara Mifugo yapata tuzo ya utawala bora

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi (sekta ya mifugo), imeshika nafasi ya pili kwenye tuzo za utawala bora zinazotolewa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kufanya vizuri kwenye upande wa utendaji bora utoaji wa huduma kwa watumishi na wananchi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Akipokea tuzo hiyo jijini Dodoma jana, kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, anayeshughulikia Sekta ya Mifugo, Tixon Nzunda, alisema tuzo hiyo imepatikana kutokana na ushirikiano mkubwa ulioko katika kufanya kazi kama timu, kwa weledi, uadilifu na uwajibikaji kwa umma.

"Nitumie fursa hii kuwashukuru watumishi wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuwezesha tuzo hii kupatikana, tumefanyiwa tathmini kwenye eneo la utawala bora ambapo tumeshika nafasi ya pili, tuchukue hii kama changamoto kwa kufanya vizuri zaidi kwenye tuzo zingine," alisema.

"Nishani hii ni kama chachu ya kufanya mabadiliko makubwa ili mwaka ujao tusiongoze tu kwenye masuala ya utawala bora, masuala ya ushughulikiaji wa malalamiko, taarifa za watumishi, lakini tuwe vinara katika kusimamia miradi ya maendeleo katika sekta zetu, kuanzia minada, mabwawa, visima, majosho, ufuatiliaji wa miradi na kuhakikisha kwamba thamani ya fedha ya miradi yetu inapatikana," aliongeza.

Awali, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Sekta ya Mifugo, Dk. Charles Mhina, alisema tuzo hiyo ya Utendaji Bora imetolewa Mei 27, 2022 kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo) kwa kufanya vizuri kwenye uingizwaji wa taarifa sahihi katika mfumo wa taarifa za utumishi na mishahara.

# Mkurugenzi Jiji la Arusha kortini tena kesi ya tatu

**Na Cynthia Mwiloleizi,**
ARUSHA

ALIYEKUWA Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Dk. John Pima (44), na wenzake watatu, jana walipandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha wakikabiliwa na mashtaka sita ya uhujumu uchumi, utakatishaji fedha na matumizi mabaya ya madaraka.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Mariamu Mshana (43) aliyekuwa Mweka Hazina wa Halmashauri ya Jiji la Arusha na Innocent Maduhu (40), aliyekuwa Mkuu wa Idara ya Mipango na Uchumi.

Katika kesi hiyo ya uhujumu uchumi namba 5 ya mwaka 2022, upande wa Jamhuri uliwakilishwa na Wakili wa Serikali Charles Kagilwa, Wakili Mwandamizi Janeth Sekule pamoja na Wakili wa Taasisi ya Kuzuia na kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Richard Jacopiyo.

Upande wa Utetezi uliwakilishwa na Valentine Nyalu na Sabato Ngogo.

Akiwasomea mashtaka hayo mbele ya Hakimu Mkazi Bitton Mwakisu, Wakili Sekule alidai watuhumiwa hao kwa pamoja kati ya Machi 23 na Mei 20 mwaka huu, wakiwa watumishi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha na waajiriwa wa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ( TAMISEMI), walifanya udanganyifu kwa kutumia nyaraka za uongo kwa ajili ya matumizi ya Sh. milioni 103 huku wakijua ni kosa kisheria.

Katika shtaka la pili, washtakiwa wote kwa pamoja Machi 27, mwaka huu wanadaiwa waliitumia nyaraka kwa nia ya kumdanganya mwajiri kwa kuweka nyaraka za uongo kwamba kulikuwa na ombi la masurufu ya kununua mchanga kwa ajili ya kutengeneza matofali huku akijua ni kosa kisheria.

Wakili Sekule alidai katika shtaka la tatu kuwa watuhumiwa hao kwa pamoja Machi 27 mwaka huu, walitumia nyaraka za uongo kumdanganya mwajiri na kuomba masurufu na malipo maalum kuwa kati ya Machi 28 mwaka huu na Aprili 14 mwaka huu, Maduhu aliomba masurufu kwa nia ya kujenga kiwanda cha matofali.

Katika shtaka la nne, ilidaiwa kuwa watuhumiwa hao kwa pamoja Machi 27 mwaka huu walitumia nyaraka za uongo kumdanganya mwajiri kuwa Maduhu ameomba mrejesho wa masurufu unaonyesha matumizi Sh. milioni 103 kwa ajili ya kufyatua matofali. Katika shtaka la tano la utakasishaji wa fedha linalomkabili Maduhu peke yake, Wakili Kagilwa alidai kuwa Aprili Mosi mwaka huu, ndani ya Jiji la Arusha, alinunua gari aina ya Subaru Forester lenye namba za usajili T 844 DYY huku akijua gari hilo ni zao la uhalifu. Akiendelea kusoma hati ya mashtaka, wakili huyo alidai katika shitaka la sita la utakasishaji wa fedha, kati ya Mei 23 na Mei 25 mwaka huu, washtakiwa walijipatia Sh. milioni 103 kwa kutumia nyaraka za uongo kumdanganya mwajiri huku wakijua fedha hizo ni zao la uhalifu.

Baada ya kusomewa mashataka hayo, washtakiwa wote walikana mashataka hayo na upande wa Jamuhuri ulidai upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika, hivyo waliomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu Mwakisu aliahirisha kesi hiyo hadi Julai 5 mwaka huu na kuamuru washtakiwa wote warudishwe mahabusu kutokana na shtaka tano na sita kutokuwa na dhamana.

**KESI MBILI ZA AWALI**

Wakati huo, Dk.John Pima na wenzake watatu wameshindwa kukidhi vigezo vya dhamana katika kesi Na. 3 na 4 za uhujumu uchumi zenye mashtaka waliyosomewa Juni 17 mwaka huu.

Watuhumiwa wengine katika kesi hiyo ni Innocent Maduhu, Nuru Ginana (40) na Alex Daniel (25), wote watumishi wa Halamshauri ya Jiji la Arusha katika Idara ya Mipango na Uchumi.

Kabla ya kuanza kwa kesi hiyo ambayo jana ilikuja mahakamani huko kwa ajili ya washtakiwa kupewa dhamana, Wakili wa Serikaki Mwandamizi Janeth aliiomba mahakama hiyo kumsomea mshtakiwa wa pili katika kesi hizo, Mariamu Mshana, mashtaka yanayowakabili kwa kuwa siku wenzake walipusomewa mashtaka yanayowakabili, hakuwapo mahakamani.

"Mheshimiwa hakimu Julai 17 mwaka huu tukiomba mahakama kutoa hati ya wito na kumkamata mshtakiwa wa pili katika kesi hizo mbili za uhujumu uchumi na leo yupo mbele ya mahakama, tunaomba kumsomea mashtaka yake ili aweze kuunganishwa na wenzake," alidai wakili huyo.

Baada ya maelezo hayo, Hakimu Mwakisu alisema kuwa kwa kuwa mshtakwa anakabiliwa na shtaka la utakatishaji wa fedha, ataendelea kuwa mahabusu na atasomewa mashtaka yake Julai Mosi mwaka huu kesi hiyo itakapokuja kwa ajili ya washtakiwa wote kusomewa maelezo ya awali.

Kuhusu dhamana za washtakiwa wengine, Wakili Nyalu anayemtetea mshtakiwa wa kwanza (Dk. Pima) alidai hajakamilisha taratibu za dhamana, huku Wakili Ngogo anayemtetea mshtakiwa wa pili (Mariamu), (Ginana) na (Daniel) akidai kuna vikwazo vimejitokeza na hivyo kusababisha kumwamisha taratibu za dhamana.

Baada ya maelezo hayo, Hakimu huyo aliagiza washtakiwa wote waendelee kubaki mahabusu hadi Julai Mosi mwaka huu.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE — BBN Limited TZA

**OMBI LA KUELEZA MASLAHI KWA UTOAJI WA HUDUMA ZA USIMAMIZI WA KODI NA SHERIA.**

**KUMB : ETJ-BB-PR-EI-JDT-EF-0001-00.**

BESIX Ballast Nedam Limited, MKANDARASI wa Uhandisi, Ununuzi na Ujenzi wa Jeti na Mitambo ya Kupakia katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Kampuni zenye uzoefu kueleza nia yao kwa ajili ya:

Kutoa usaidizi, ushauri na huduma kuhusu masuala mbalimbali ya usimamizi wa kodi na sheria zinazohusu UHANDISI, MANUNUZI NA UJENZI (EPC) WA GATI YA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP) na shughuli za kampuni na biashara za kila siku nchini Tanzania.

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Kama sehemu ya mradi wa EACOP, mafuta ghafi yatapakiwa kwenye meli kupitia kituo kilicho karibu na ufukwe wa Bahari ya Hindi. Kituo hiki kitakuwa umbali wa kilomita 2 kutoka ufukweni kutoka eneo la Hifadhi ya Bahari lililopo kwenye peninsula ya Chongoleani mbele ya Bandari ya Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA/HUDUMA:**
- Kutoa huduma kwa ubora wa hali ya juu, gharama nafuu, uwakilishi mzuri na ushauri wa kisheria kwa wakati.
- Ukaguzi na huduma na usimamizi wa viashiria hatarishi,
- Kutoa huduma za kihasibu na utengenezaji wa hati za malipo.
- Kutoa usaidizi katika kodi za moja kwa moja, zisizo za moja kwa moja, gharama za miamala ya fedha na utatuzi wa migogoro.

**SIFA BAINIFU:**
Makampuni yenye nia yanaalikwa kuwasilisha maombi yao kwa kuambatanisha nyaraka zifuatavyo:
- Leseni za biashara au uthibitisho kutoka mamlaka husika,
- uzoefu usiopungua miaka 5 katika kutoa huduma zinazohitajika na zilizo ainishwa,
- Timu ya wahasibu wa umma (CPA) walioidhinishwa, wanasheria na washauri wa kodi walio na uzoefu katika maeneo yafuatayo ya sheria: biashara, mashirika, usimamizi wa fedha, kodi na usimamizi wa kesi za madai/fidia.
- Uwezo wa kutosha wa kifedha kufanya au kusimamia kandarasi husika.
- Uzoefu wa kutoa huduma kamili na kufanya kazi na wateja au makampuni ya kimataifa.
- Kuzingatia kanuni za petroli (matumizi ya rasilimali za ndani),2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha jibu kwa usemi huu wa maslahi unapendekezwa sana.
- Kuzingatia kanuni za Matumizi ya rasilimali za ndani (Local Content) za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha nia, unashauriwa.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji ya chini kabisa na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu wanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu kwa **procurement@bbnjv.com** **(Ukubwa wa Barua Pepe na viambatanishi: MB 20 & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya tarehe **6 Julai 2022 , Saa 12 jioni kwa saa za Tanzania,**

Makampuni yatakayokidhi vigezo yatatathminiwa na ikiwa yatachaguliwa yataalikwa, kulingana na Makubaliano ya Kutofichua Mkataba (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka :** Kampuni zilizokidhi matakwa ya awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa Wito wa Zabuni.

216913201



EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE — BBN Limited TZA

**REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST FOR THE PROVISION OF Quick Release Hooks**

**REF : ETJ-BB-PR-EI-JDT-EF-0001-00.**

BESIX Ballast Nedam Limited, the CONTRACTOR for the Engineering, procurement and Construction of the Jetty and Load Out Facilities in the Tanga Bay for the East African Crude Oil Pipeline (EACOP) Project, invites experienced specialist Companies to express their interest for:

Design, Fabrication, Testing, Supply, Delivery and on-site inspection of Quick Release Hooks.

The Republic of Uganda, the Uganda National Oil Company (UNOC), the United Republic of Tanzania and/or Tanzania Petroleum Development Corporation (TPDC), as well as other international oil companies are partaking in the implementation of the EACOP Project.

As part of EACOP project, the Crude oil will be loaded on vessels via a facility located in the near shore environment of the Indian Ocean. The Facility will be located 2 km offshore from the Marine Storage Terminal site located on the Chongoleani peninsula in front of Tanga Port in Tanzania.

**BRIEF DESCRIPTION OF THE SCOPE OF THE MATERIALS / SERVICES:**
- Triple and double electric-release Quick Release Hooks with integral single speed capstan and accessories,
- Cast inserts for each Hook,
- Jetty monitoring and control junction box,
- Central control cabinet, incl. UHF/DGPD antennas + cabling,
- Hooks bases are coated,
- Transport FOB incoterms Liner out.

**MINIMUM REQUIREMENTS:**
Companies expressing their interest are invited to document their request with :
- Qualified workers and certified QA/QC ;
- Fabrication at fabrication yard, not on site ;
- Coating from Carboline, Hempel, Jotun or PPG ;
- Company profile with prove of sufficient financial capabilities and sufficient and capable resources.
- An experience list with relevant supply history / track record showing minimum of five (5) years' experience in execution similar services of required fabrication and transport as per international standards common in the Oil and Gas business or comparable market,
- Applicable codes: BS6349-4 (2014) and OCIMF (Mooring Equipment Guidelines);
- Company's Quality and HSE plans and certification : ISO 9001:2015, ISO 14001:2015, OHSAS 18001 (ISO45001:2018) or equivalent certificates ;
- CE marked as per CPR and BS EN 1090 ;
- Compliance with petroleum (local Content) regulation of 2017 and local company definition for Tanzania.
- Proof of registration/application to Local Supplier Service Provider (LSSP) database at the time of submission of the response to this expression of interest is highly recommended.

Interested companies which meet the minimum requirements and have the capacity to provide the services listed above should express their interest by sending together with the above listed documents an email to **procurement@bbnjv.com** **(Max. Email Size: 20 MBs & All documents must be submitted in the English language)** on or before **6th of July 2022, 12 noon Tanzania Time,**

Companies satisfactorily meeting the above minimum requirements will be evaluated and if selected will be invited, subject to the signature of a Non-Disclosure Agreement (NDA), to participate in the bidding process.

**Note:** Only pre-qualified companies will receive an invitation to submit their bid in furtherance of the Call for Tender process.

216913201

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mpango wa kutambua wabunifu uwe chachu ya kuibua wengi zaidi

SERIKALI imeanza utaratibu wa kuwatambua wabunifu nchini kupitia mashindano kutokana na kuwapo kwa mwongozo wa kutambua na kuendeleza ubunifu na maarifa asilia.

Katika mwongozo huo wabunifu 2,647 wametambuliwa na kuibuliwa katika mashindano ya Kitaifa ya Sayansi,

Teknolojia na Ubunifu (Makisatu) ndani ya miaka minne tangu mwaka 2018.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwasasa inafanya mapitio ya rasimu ya mwongozo huo ili kukidhi mahitaji yaliyoko kwa kuibua wabunifu wengi zaidi na kuwaendeleza.

Imeelezwa kuwa bila kuwapo na sayansi, teknolojia na ubunifu, maendeleo yanayotamaniwa nchini ni ngumu kuyafikia.

Nchi nyingi duniani zinaendelea kutokana na kujikita katika sekta ya sayansi na teknolojia ndivyo dunia inavyokwenda kwa sasa.

Imeshauriwa mapitio ya mwongozo huo yalenge kuwapo kwa hamasa ili wabunifu waonyeshe ubunifu wao.

Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko kwa baadhi ya wabunifu kutothaminiwa kazi zao au kupata ushirikiano ili kuziendeleza, hali inayowakatisha tamaa.

Kupitia mwongozo huo tuna imani kuwa watu wengi wenye vipaji vya ubunifu watapata fursa ya kuonyesha kazi zao na hatimaye kufikia malengo waliyojiwekea.

Kati ya wabunifu hao waliotambuliwa imeelezwa kati yao 283 wameendelezwa na wapo kwenye hatua mbalimbali huku zaidi ya 26 bunifu zao zikifikia hatua ya kutangazwa kibiashara.

Vikwazo kadhaa vinavyosababisha kutokuwa na wabunifu wengi vimeelezwa kuwa ni suala la mtazamo na uelewa wa masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

Pia, kazi zinazobuniwa zinatakiwa kuwa na hatimiliki ili kulinda haki ya mtu isiibiwe na hilo linahitaji elimu ya kutosha kwa wabunifu wetu.

Baadhi ya watu wanaokwamisha wabunifu kusonga mbele ni wanaotoa vikwazo zikiwamo leseni, wakati mbunifu akiwa ndiyo kwanza ameanza kazi hiyo.

Ubunifu ni suala linalomfanya mtu kutumia akili na maarifa ili kitu atakachokibuni kiweze kukubalika mbele ya watu wengine na kuleta tija.

Tunasema hatua inayochukuliwa na serikali kupitia Mkurugenzi wa Idara ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu wa Wizara hiyo, Prof. Maulilio Kipanyula, ya kuboresha mwongozo huo ili kuongeza hamasa, kuibua, kutambua na kuendeleza ubunifu hasa kwa ngazi za chini ni wa busara, unatia moyo.

Kwa mujibu wa serikali rasimu ya mapendekezo ya mwongozo huo itajadiliwa na kikosi kazi na kutoa maoni ili kukamilisha mapitio ya mwongozo huo.

Dhamira ya serikali kupitia wizara hiyo ni kuhakikisha mwongozo unaboreshwa ili kukidhi mahitaji ya sasa kutokana na mwongozo wa awali kuwa na upungufu ikiwamo kutoonesha majukumu ya wadau katika kuibua, kutambua na kuendeleza wabunifu.

Ni muhimu kwa vijana ambao kila kukicha wanalia kukosekana kwa ajira wakatumia fursa hii kubuni vitu vitakavyowawezesha kujiajiri.


Mwongozo huo unatoa fursa ya bunifu zitakazoibuliwa kutangazwa kibiashara ili kuleta tija kwa wabunifu hao.

Ni vyema suala hilo likatolewa elimu ya kutosha ili kulinda wabunifu wetu na kuweza kufanyakazi vizuri zaidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# CCM iwatose wanaodai kutumwa na viongozi

Na Sabato Kasika

**CCM** inaendelea na uchaguzi wa viongozi wa chama hicho na jumuiya zake za Umoja wa Wanawake UWT na Umoja wa Vijana -UVCCM ngazi ya kata baada ya kumaliza ule wa mashina na matawi ulioanza Aprili mwaka huu.

Wakati uchaguzi huo ukiendelea kumekuwa kukiibuka figisu mbalimbali zenye lengo la kukwamisha baadhi ya makada kuwania nafasi katika chama na jumuiya ambazo hata hivyo zilishashtukiwa.

Miongoni mwa figisu zilizoshtukiwa ni zile za kuwanyima fomu za kuwania uongozi baadhi ya makada, hali iliyosababisha Katibu Mkuu wa chama hicho, Daniel Chongolo, kuingilia kati na kuagiza utoaji fomu urudiwe.

Wakati uchaguzi ukiendelea, katibu huyo amegundua mbinu nyingine zinazotumiwa na baadhi ya makada kwa lengo la kutaka kufanikisha kupata nafasi za uongozi na kuwataka kuacha mara moja.

Anabainisha kuwa, wapo wagombea wa nafasi mbalimbali ndani CCM, ambao wanatumia majina ya viongozi wakuu kwamba wamewatuma kugombea, jambo ambalo anasema halina ukweli wala msingi.

Ni wakati akifungua kikao cha Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake UWT, jijini Dodoma, anasema hayo huku akiongeza kuwa ni aibu mtu mzima kutumia jina la kiongozi wake kuwa amemtuma.

Ninaungana na katibu huyo kwa kauli yake hiyo, kwani mbinu hizo zinaweza kusababisha kupata viongozi ambao si chaguo la wanachama, hivyo ni vyema kada achaguliwe kulingana na sifa zake si kutumia mgongo wa mtu mwingine.

Kimsingi, kiongozi mwenye dhamira ya kuongoza chama anachaguliwa kulingana na sifa zake kama ambavyo chama kitamtathmini badala ya kusingizia wakubwa wa chama kuwa wamemtuma awanie uongozi.

Hivyo, ninadhani onya la Chongolo lingetosha kuwarudisha katika mstari wale wote ambao wanatarajia kutumia majina ya viongozi wakubwa kufanikisha mikakati yao ya kuwania uongozi wa CCM na jumuiya zake.

**Hivyo, wakati uchaguzi ukiwa umefikia ngazi ya kata, ni vyema makada wakazingatia maelekezo ya Katibu Mkuu wa chama hicho ili kuwakwepa wale**

Ninaamini kwamba kada mwenye nia ya kweli ya kuongoza, atajinadi mwenyewe bila kutumia jina la kigogo yeyote, hivyo anayesubiri kubebwa, ninadhani hawezi kuwa na sifa za kuwa kiongozi bora.

Sidhani kama ni sahihi kada wa chama kusimama na kumtaja kiongozi kuwa amemtuma kuwania uongozi. Hiyo ina maana kwamba hana nia ya kuongoza ila anafanya hivyo kwa sababu ametumwa na kiongozi.

Kwa mazingira kama hayo, ni vyema wanachama wakawa makini kuwakwepa wagombea wa aina hiyo, lakini kama kuna viongozi wanaowabeba au kuwatuma, basi wasifanye hivyo kwa maslahi ya chama.

Waswahili wana msemo wao kuwa kizuri chajiuza, kibaya chajitembeza, hivyo makanda wangezingatia kizuri ambacho kinajiuza chenyewe badala ya kile kinachojitembeza kwa kujitangaza kuwa kimetumwa.

Hivyo wakati huu wa uchaguzi wa ngazi ya kata na kisha wilaya, ni vyama wanachama CCM msiwachague wanaodai kutumwa na viongozi badala yake mchague wenu si wale wa kutumwa.

Kama ambavyo Chongolo aligusia kuwa kiongozi mwenye dhamira njema ni yule anayesimama kwa miguu yake, nami naamini katika hilo, kwani anakuwa na nia ya kweli ya kukitumikia chama.

Ni kweli kwamba, kada anayedhamiria kuwa kiongozi, hahitaji kuwa na mguu wa pembeni wa kumsaidia kugombea nafasi, badala yake anasimama mwenyewe kwa miguu yake miwili kuomba kura kwa wanachama wenzake.

Hivyo, wakati uchaguzi ukiwa umefikia ngazi ya kata, ni vyema makada wakazingatia maelekezo ya Katibu Mkuu wa chama hicho ili kuwakwepa wale wote wanaojinadi kwa mgongo wa wengine.

## Zaidi ya wabunifu 2,000 watambuliwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WABUNIFU 2,647 wametambuliwa na kuibuliwa kupitia mashindano ya kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (Makisatu) ndani ya miaka minne tangu kuwapo kwa mwongozo wa kutambua na kuendeleza ubunifu na maarifa asilia wa mwaka 2018.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inafanya mapitio ya rasimu ya mwongozo huo ili kukidhi mahitaji yaliyopo kwa kuibua wabunifu wengi zaidi na kuwaendeleza.

Prof. Mdoe alitoa kauli hiyo jana kwenye kikao cha wadau wa mapitio ya rasimu ya mwongozo huo, jijini hapa.

Alisema bila kuwapo na sayansi, teknolojia na ubunifu maendeleo yanayotamaniwa nchini ni ngumu kuyafikia.

Alihimiza mapitio ya mwongozo huo yalenge kuwapo kwa hamasa ili wabunifu waoneshe ubunifu wao.

"Tangu uwapo mwongozo huu tumeibua wabunifu wengi tumewatambua wapo 2,647 hawa tumewaibua kupitia mashindano maarufu ya Makisatu, tumewatambua ndani ya miaka minne naamini wapo wengi zaidi ya hao," alisema.

Alisema kati ya hao 283 wameendelezwa na wapo kwenye hatua mbalimbali huku zaidi ya 26 bunifu zao zikifikia hatua ya kutangazwa kibiashara.

Alizungumzia vikwazo kadhaa vinavyosababisha kutokuwa na wabunifu wengi ni suala la mtazamo na uelewa wa masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

Kuhusu wathibiti, Prof. Mdoe alisema shughuli za uthibiti ubora wa bunifu sheria zilizounda mamlaka husika za masuala hayo zipo kipolisi na hazihamasishi ubunifu.

"Mtu akija na kitu chake cha ubunifu kitu cha kwanza una leseni, umelipia huyu ndiyo kwanza ameanza kubuni hakijaanza kufanya kazi, atakijaribu vipi wewe unataka alipie ndiyo ajaribu, lazima tuwe wawezeshaji kuhamasisha ubunifu sio kudhibiti badala ya kuthibiti," alisema.

Naye, Mkurugenzi wa Idara ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu wa Wizara hiyo, Prof. Maulilio Kipanyula, alisema lengo la kuboresha mwongozo huo ni kuongeza hamasa, kuibua, kutambua na kuendeleza ubunifu hasa kwa ngazi za chini.

Alisema rasimu ya mapendekezo ya mwongozo huo itajadiliwa na kikosi kazi na kutoa maoni ili kukamilisha mapitio ya mwongozo huo.

Prof. Kipanyula alisema dhamira ya wizara ni kuhakikisha mwongozo unaboreshwa ili kukidhi mahitaji ya sasa kutokana na mwongozo wa awali uliokuwa na upungufu ikiwamo kutoonesha majukumu ya wadau katika kuibua, kutambua na kuendeleza wabunifu.

# Wakulima, wafugaji wapewa mbinu za kuepuka migogoro

**Na Idda Mushi,** KILOSA

WAFUGAJI na wakulima wilayani Kilosa, mkoani Morogoro, wameanzishiwa mradi wa kuwajengea uwezo wa kilimo endelevu na ufugaji bora kwa kutengewa zaidi ya ekari 100 za malisho ya mifugo ili kupunguza na kumaliza migogoro baina yao.

Akizungumza katika kijijini cha Mbwade kata ya Madoto Ranchi, wilayani Kilosa kwenye makabidhiano ya mbegu bora 16 za ng'ombe na saba za mbuzi, Mkurugenzi wa Shirika la Kilimo Endelevu Tanzania (SAT), Janet Maro, alisema kupitia mradi huo wamelenga kuleta ushirikiano kati ya wakulima na wafugaji ili kupunguza migogoro.

Alisema ugawaji wa mbegu za ng'ombe na mbuzi kwa wafugaji ulifanyika kwa kutoa elimu ili wafugaji waweze kufuga na kuzalisha mifugo mingi yenye tija itakayowasaidia kuongeza kipato chao na taifa kwa ujumla.

"Tumetenga zaidi ekari elfu moja kwaajili ya malisho Ili yasaidie wafugaji kulisha mifugo yao hasa wakati wa kiangazi ili isife kutokana na kukosa chakula kwa kipindi kirefu," alisema Maro.

Alisema, wameanzisha mashamba hayo ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambayo kwa sasa yanaathiri shughuli za kilimo na ufugaji hasa kwa wanaofanya kwa mazoea.

Wawakilishi kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Sebastian Shilangalila, aliwapongeza SAT kwa kazi inayofanya ya kuelimisha wafugaji kufuga kisasa na kuondokana na migogoro kati yao na wakulima.

Mwenyekiti wa wafugaji wa Wilaya ya Kilosa, Mkunwa Suhani, akizungumza kwa niaba ya wafugaji, alisema ujio wa mbegu hizo utaleta mageuzi makubwa kwa wafugaji kwa kuwa awali walikuwa wanafuga kienyeji na kusababisha mifugo mingi isiyo na tija na migogoro.

Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Majid Mwanga, akizungumza wakati wa kupokea na kukabidhi mbegu za mifugo, aliwataka wafugaji wilayani humo kuacha mara moja tabia ya kujichukulia sheria mkononi kwa kufanya fujo kwenye mashamba ya wakulima na kuwacharaza viboko wakulima wanaolalamikia mashamba yao kuvamiwa na mifugo.

Aliwahimiza wakulima na wafugaji kuungana pamoja kutokomeza migogoro ya wakulima na wafugaji ambayo imekuwa kero katika wilaya hiyo na kuonya baadhi ya wafugaji wanaokimbilia maeneo mengine kupeleka malalamiko na kuwaacha viongozi wa wilaya bila kufahamu kinachoendelea au wakiamini wanaonewa.




Mwenyekiti mstaafu wa Baraza la Biashara la Afrika Mashariki (EABC), Nick Nesbit (kushoto), akimpongeza Mwenyekiti mpya wa baraza hilo, Angelina Ngalula, baada ya kuchaguliwa na Bodi ya EABC kushika wadhifa huo, jijini Kigali, nchini Rwanda jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB yatoa msaada wa mabati ujenzi zahanati

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

BENKI ya NMB imetoa msaada wa mabati 200 yenye thamani ya Sh. milioni 8.5 kwa ajili ya ujenzi wa zahanati katika kijiji cha Ivilikinge kilichoko wilayani Makete, mkoani Njombe.

Akizungumza baada ya kukabidhi mabati hayo, Meneja wa benki hiyo Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Straton Chilongola, alisema walipopata maombi ya kuchangia maendeleo katika wilaya hiyo walifarijika na kuamua kushiriki kuchangia kwenye sekta hiyo muhimu katika jamii.

"Vifaa hivi tunavyokabidhi leo ni moja ya ushiriki wetu katika maendeleo ya jamii na tunao wajibu wa kuhakikisha kuwa jamii inayotuzunguka inafaidika na faida tunayoipata," alisema Chilongola.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Makete, Juma Sweda, baada ya kupokea msaada huo alisema utekelezaji wa mradi huo wa ujenzi wa zahanati utafanyika haraka iwezekanavyo ili wananchi wa kijiji hicho waweze kunufaika na huduma za afya.

Aliiomba benki hiyo kutoa msaada mwingine wa vitanda ili kuboresha zahanati hiyo ili wajawazito waweze kujifungua salama. "Kwa kuwa zahanati hii itaisha niwaombe mtuongezee vitanda na tukishafanya hivyo kinamama wapo wanataka kujifungua na wapo tayari kushika mimba na serikali ya mama Samia inasema kushika mimba na kijifungua ni bure," alisema Sweda.

Mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Abia Sanga, aliwashukuru NMB kwa msaada huo na kwamba zahanati iliyopo sasa ni chakavu na yenye miundombinu duni iliyojengwa zamani kiasi cha kushindwa kuendana na mahitaji ya sasa ya utoaji huduma za afya hasa za uzazi salama.

Kwa upande wa Furaha Sanga alisema jengo la zahanati hiyo ni dogo na kusababisha mrundikano wa wagonjwa wengi hadi wengine kukosa sehemu ya kupumzishwa baada ya kupata matibabu.

# Wazee CCM wataka wastaafu wamuunge mkono Dk. Mwinyi

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI mstaafu wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Mjini na Magharibi Unguja, Boraafya Sirima Juma, amewataka viongozi wastaafu ndani ya chama kuunga mkono juhudi na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi katika kuleta mageuzi ya kiuchumi na kuinua maisha ya Wazanzibar wote.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini hapo jana, Juma alitoa wito kwa wastaafu kuiunga mkono serikali na kukemea vitendo vya baadhi ya wastaafu ndani ya CCM kuwa kikwazo kwa viongozi katika kutekeleza majukumu yao.

"Kustaafu siyo dhambi, ni vizuri na jambo ambalo lipo kisheria. Wapo watu wasiokubali kustaafu wala kuamini kuwa kila zama kitabu chake pamoja na watu wake. CCM ni chama chenye misingi imara sana na kinaongozwa kwa katiba na kanuni zake," alisema.

Juma aliongeza kuwa haoni sababu ya kuleta vurugu ndani ya chama wakati zipo taratibu za kufuata. Alisema hatua zinazochukuliwa na viongozi wa kitaifa akiwamo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Mwinyi na Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, zina baraka zote za chama na pia ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya CCM.

Aliwakumbusha wana-CCM kuwa vyama vya TANU na ASP kabla ya kuungana mwaka 1977, vilijielekeza katika suala la ukombozi lakini kuundwa kwa CCM kulilenga kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii na ndicho kinachofanyika sasa.

"Rais mstaafu wa Zanzibar, Dk. Salmin Amour alipofanya uamuzi wa kujenga hoteli, alipingwa sana na baadhi ya watu bila kujua matokeo ya baadaye, lakini leo matunda ya uwekezaji huo yanaonekana na serikali inapata mapato mengi katika eneo hilo," alisema.

Juma aliwataka wana-CCM kuendelea kumuunga mkono Rais wa Zanzibar na yule wa Jamhuri ya Muungano ili serikali zao ziweze kutekeleza ilani ya uchaguzi kwa kuwaletea Watanzania maendeleo stahiki ya kijamii na uchumi.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa wa Kaskazini Pemba, Ramadhani Shaibu Juma, alikemea habari za upotoshaji kuwa Rais ameuza visiwa kwa kuwa siyo za kweli kwani kilichofanyika ni kuhamasisha uwekezaji kwenye fukwe ili kuchochea ukuaji wa uchumi.

"Sisi Zanzibar hatuna madini zaidi ya uchumi unaotokana na mazao ya bahari na kilimo. Kuhamasisha uwekezaji kwenye fukwe utasaidia kuongeza vipato kwa wakazi wa maeneo husika," alisema.

"CCM lazima turudi kwenye maadili ya chama. Sisi wa-NEC tuna jukumu kubwa la kuimarisha chama sambamba na kulinda maadili kuanzia ngazi ya tawi hadi Taifa," alisema na kuzipongeza serikali mbili kwa kazi nzuri inayofanywa kuwaletea wananchi maendeleo.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Omar Zubeir Mbwana, alisema ubinafsi miongoni mwa watu wachache ambao pia wanakiuka ahadi zao kwa chama, ni chanzo cha malumbano yasiyo na tija.

"Chama lazima kiyafuatilie magenge ya wanachama ndani ya chama na wale wote wanaothibitika kukiuka maadili na misingi ya chama, ni vizuri wakachukukuliwa hatua stahiki za kinidhamu ili kukomesha tabia hizo," alisema.



Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania (TRCS), Tryphone Mkolokoti, akimpa msaada wa fedha mmoja wa waathirika wa ukame wilayani Longido mkoani Arusha, ambapo kaya 1,200 zimefaidika na msaada huo, huku kila moja ikipata Sh. 140,000. Kulia ni Kaimu Ofisa Maafa wa Longido, Albert Israel na Meneja wa Maafa wa TRCS, Samuel Katamba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## RC: Wafanyabiashara watoe ushirikiano TRA

**Na Mwandishi Wetu,**
SONGWE

MKUU wa Mkoa wa Songwe, Omari Mgumba, amekutana na maofisa wa Mamlaka ya Mapato (TRA) na kuishukuru mamlaka hiyo kwa kuwatembelea walipakodi wa Mkoa wa Songwe kwa ajili ya kutoa elimu mlango kwa mlango.

Amesema uamuzi huo wa kuwatembelea wafanyabiashara utasaidia kupata uelewa mpana kwa wafanyabiashara wa Songwe kujua wajibu wa mamlaka na wajibu wa walipakodi.

Kiongozi huyo alibainisha hayo jana mkoani hapo alipozungumza na maofisa hao.

Mkuu wa Mkoa aliwataka wafanyabiashara kutoa ushirikiano wa dhati kwa maofisa hao ili kupata elimu ya kodi na kuhakikisha wanasimamia maneno na maelekezo ya serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan bila kutumia nguvu, mabavu na hila.

Alisema TRA imekuwa ikikusanya kodi kwa weledi na kukutana na wafanyabiashara kuwapa elimu ili kujua umuhimu wa kodi na madhara ya ukwepaji kodi.

Vilevile, alitoa rai kwa wafanyabiashara wanapouza bidhaa, watoe risiti na mnunuzi kudai risiti kwa kuwa kutokufanya hivyo ni kuikosesha mamlaka na serikali mapato yake halali na kudhoofisha juhudi za serikali.

Meneja wa Songwe wa TRA, Dickson Kimaro, alisema ujio wa maofisa hao kutoka makao makuu utasaidia ongezeko la ukusanyaji wa mapato na kuondoa kero walizokuwa nazo walipakodi katika mkoa huo wa Songwe.

Ofisa Uhusiano Mkuu, MacDonald Mwakasindile kutoka TRA Makao Makuu, alisema utaratibu huo wa kutoa elimu ya kodi mlango kwa mlango unalenga kutoa huduma kwa wafanyabiashara ili kuangalia jinsi wanavyolipa kodi.

# Serikali kuwezesha DMI vifaa vya kisasa

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imeahidi kukiwezesha Chuo cha Bahari (DMI) cha jijini Dar es Salaam kwa miundombinu bora na vifaa vya kisasa vya kufundishia ili kiweze kuwa na viwango vya kimataifa.

Ahadi hiyo ilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, wakati akifungua kongamano la kwanza la uchumi wa buluu.

Kongamano hilo lililoandaliwa na DMI ni la kwanza kufanyika nchini kuhusu uchumi wa buluu na maudhui yake ni 'kuibua fursa zitokanazo na bahari kwa maendeleo ya taifa'.

Naibu Waziri huyo alisema eneo kiliko chuo hicho Posta, Dar es Salaam ni dogo, hivyo serikali inaangalia uwezekano wa kutenga eneo kubwa kwenye Mkoa wa Pwani kwa ajili ya kupanua shughuli za chuo hicho.

Alisema kwa kuanzia, serikali imeshatenga Sh. bilioni moja kwa ajili ya ununuzi wa mfumo wa kufundishia manahodha wa meli inayofahamika kama Stimulators.

"Niliwahi kutembelea hiki chuo hivi karibuni na kwa kweli nilijionea mwenyewe miundombinu ilivyo chakavu lakini mkakati uliopo ni kukiwezesha kuwa cha kisasa na kitakuwa na majengo yenye viwango na tayari wana maeneo Mkoa wa Pwani," alisema Mwakibete.

Mwenyekiti wa Bodi ya DMI, Ernest Bupamba, aliiomba serikali iiangalie DMI kwa jicho la huruma ikizingatiwa kuwa ndicho chuo pekee kinachotoa mafunzo ya bahari nchini.

Alisema chuo hicho ndicho pekee kinazalisha rasilimali watu inayohitajika kwenye uendeshaji wa uchumi wa buluu, hivyo iwapo kitawezeshwa kwa vifaa na majengo, kitatoa mchango mkubwa kwenye kufikia malengo.

Pia aliishukuru Serikali ya Visiwa vya Shelisheli kwa namna ambavyo imeisaidia Tanzania katika kupambana na vitendo vya uvuvi haramu kwenye bahari yake.

Alisema mara kadhaa viongozi wa serikali hiyo wamekuwa wakiwasiliana na Serikali ya Tanzania kila wanapoona wavuvi haramu na kisha vyombo vya usalama kwenda kuwakamata na kuwafikisha kunakohusika kwa hatua za kisheria.

"Ni mara nyingi sana Shelisheli imekuwa msaada mkubwa kwa Tanzania kwa sababu kule watu wamekuwa wakijaribu kufanya uvuvi haramu, lakini kila wakijaribu wanatupigia simu na serikali yetu inachukua hatua haraka sana na imesaidia kwa kiasi kikubwa," alisema.

Kaimu Mkuu wa chuo hicho, Dk. Tumaini Gurumo, alisema kwa mwaka chuo hicho kinazalisha mabaharia 100 ambao wanakidhi soko la ndani na wengine wanakwenda kufanya kazi nje ya nchi.

"Soko la mabaharia ni kubwa sana. Sisi tunazalisha 100 kwa mwaka ambao wanakidhi mahitaji ya ndani na wengine wanakwenda kufanya kazi nje ya nchi, vijana wachangamkie fursa hii kwa sababu ina fedha za kutosha na ajira yake siyo ya kuhangaika," alisema Dk. Tumaini.

## Msalaba Mwekundu yasaidia watoto wenye utapiamlo

**Na Yasmine Protace**

CHAMA cha Msalaba Mwekundu Tanzania (TRCS), kimetoa msaada wa vyakula kunusuru watoto dhidi ya utapiamlo na Sh. milioni 16.8 kwa familia zilizoathiriwa na ukame katika mikoa ya Arusha na Manyara.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu Taifa wa chama hicho Tanzania (MNEC-TRCS), Tryphone Mkolokoti, aliiambia Nipashe kuwa vyakula hivyo vinajumuisha ungalishe, ndizi mbivu na machungwa na dawa.

"TRCS imetoa msaada wa fedha kwa kaya 1,200 katika wilaya hizo, kila kaya ilipata Sh. 140,000 na kaya 150 zimepata msaada wa ungalishe, matunda na dawa na kufundishwa jinsi ya kupika," alisema Mkolokota.

Alisema, msaada huo ulitolewa mwishoni mwa wiki katika wilaya za Longido na Monduli, mkoani Arusha, Simanjiro na Mbulu mkoani Manyara.

Mkolokoti aliyemwakilisha Rais wa TRCS ambaye ni Mbunge wa Mufindi Kusini mkoani Iringa, David Kihenzile, aliipa pole jamii ya kifugaji kwa kupoteza mifugo kutokana na ukame na kuahidi kushirikiana nayo.

"Tutaendelea kuwa nanyi wakati wa maafa na hata wa raha, hivyo ninawaomba mwendelee katika imani ya TRCS muwe wanachama wa mfano, ili kuwa karibu katika shughuli za kusaidiana pale mnapohitajika," alisema.

MNEC huyo alifafanua kuwa hiyo ni mara ya pili kwa chama kutoa msaada katika mikoa ya Arusha na Manyara, mara kwanza walitoa fedha kwa kaya 700 za wilaya za Longido, Simanjiro na Mbulu.

"Kila kaya ilipata Sh. 140,000, mwezi ujao wa Julai tutakwenda tena kutoa msaada, dawa na vyakula vyenye virutubishi muhimu kwa watoto wa chini ya miaka mitano kutoka jamii ya kifugaji," alisema.

Mkolokoti alisema, TRCS imekuwa ikitoa msaada huo kwa familia hizo zinazokumbwa na ukame na kusababisha watoto kupata utapiamlo, na kwamba ni muhimu kufanya kila njia kuwanusuru.

Alifafanua kuwa TRCS imekuwa ikifanya kazi zake katika maeneo mbalimbali ndani ya jamii, kwa ufadhili wa Shirikisho la Kimataifa la Vyama vya Msalaba Mwekundu (IFRC).

# COSTECH kutengeneza mazingira kuwezesha vijana

**Na Elizabeth Zaya**

TUME ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), imesema itaendelea kutengeneza mazingira mazuri ya kuwawezesha wanasayansi wengi hususani vijana ili utafiti unaofanywa upate fursa ya kuingizwa kwenye biashara.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi wa COSTECH, Emmanuel Mgonja, wakati akifungua mradi wa kuwawezesha wanafunzi wanasayansi kutoka katika shule mbalimbali za sekondari Dar es Salaam namna ya kubuni miradi ya kibiashara unaoratibiwa na Taasisi ya Dar Teknohama Business Incubator (DTBi).

Mgonja alisema, wanasayansi wengi wanaishia kwenye kutafiti vitu kwa namna ya kinadharia na imefika wakati sasa hivyo wanavyovitafiti au kuvibuni waviingize katika matendo ili visaidie kutatua matatizo mbalimbali katika jamii.

"Na ndiyo maana tunaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wanasayansi hawa kuanzia shuleni ili wawe wanafanya tafiti ambazo watazitumia kwenye fursa mbalimbali za kibiashara, hatutaki tafiti zao ziwe zinaishia kwenye nadharia tu," alisema Mgonja.

"Tunataka wanasayansi hawa wawe wanatafiti changamoto mbalimbali zilizopo kwenye jamii zao na kuleta majawabu kwa vitendo, kwa kuzigeuza kuwa fursa na kufanya hivyo kutawasaidia kupambana na tatizo la ajira. Kuna changamoto kwa wanasayansi kufanya sana tafiti, lakini wao hawazitumii kwenye fursa za kibiashara."

Alisema wanataka taaluma ya sayansi ambayo wanafunzi wanaipata iwasaidie kujiingiza kwenye biashara.

Kwa upande wake, Josephine Sepeku, ambaye ni Meneja Mradi huo unaojulikana kama future stem business leaders Tanzania, alisema waliuanzisha kwa lengo la kuhakikisha wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi waitumie kihalisia kutatua matatizo yaliyoko katika jamii.

"Na tangu tumeanza mradi huu mwaka 2017, tumeanza kuona matunda mazuri. Kwa mfano mwaka jana kuna wanafunzi ambao walifanya tafiti za miradi mbalimbali na iliposhindanishwa ilishinda, na ilikuwa ni miradi ambayo ilikuwa ni changamoto katika jamii yao," alisema Sepeku.

"Lengo ni kuona zile sayansi za darasani wanazopata wanafunzi, wanazitumia kwenye uhalisia, tunataka, mwanafunzi anapoona tatizo kwenye jamii yake, aitumie kama fursa kwenye biashara."

Mkuu wa Idara ya Fizikia wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Nuru Mlyuka, alisema wanajitahidi kutoa tafiti ambazo zina matokeo chanya kwa jamii na sio kubaki kwenye nadharia.




Kaimu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale mkoani Geita, Leonard Bathromeo Mgema (aliyevaa koti), akitoa ripoti kwa maofisa waandamizi wa mgodi wa Barrick Bulyanhulu waliotembelea miradi ya maendeleo iliyofanikishwa na fedha za kusaidia jamii zilizotolewa na mgodi huo (CSR) wilayani humo. Wapili kushoto ni Meneja Mkuu wa Barrick Bulyanhulu, Cheick Sangare. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vituo vya afya vyaonywa udanganyifu vipimo

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

VITUO binafsi vya huduma za afya mkoani Mtwara vimeonywa tabia ya kutoa vipimo vya uongo kwa wateja wao na watakaobainika serikali itawachukulia hatua kali za kisheria ikiwa ni pamoja na kufuta leseni ya uendeshaji.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Dk. Hamadi Nyembea, alitoa onyo hilo alipokuwa akizungumza na watoa huduma za afya wa mkoa huo kwenye kikao kazi cha kujifunza namna ya kuendesha vituo hivyo pamoja na kuelewa jinsi ya kusajili kituo cha kutolea huduma za afya.

Alisema kuna baadhi ya vituo vya afya vyenye tabia ya kupima magonjwa hasa wa malaria na kutoa majibu ya uongo kwa wateja wao ili kujipatia fedha.

Dk. Nyembea alisema, kuanzia sasa tabia hiyo ikomeshwe mara moja na ufuatiliaji wa kituo kwa kituo na ukaguzi wa vifaa vinavyotumika kwenye vituo hivyo ufanyike ili kujiridhisha na ubora wa vifaa hivyo.

Alisema kitendo cha kutoa vipimo visivyokuwa vya ukweli kwa mgonjwa ni kosa kisheria na hatari kwa aliyepata huduma kwenye kituo.

Aliagiza kila kituo lazima kifuate kanuni na utaratibu mzuri wa kitabibu ikiwa ni pamoja na kupima na kutoa vipimo sahihi vya ugonjwa.

"Tumefanya ukaguzi wa kawaida wa siri kwenye baadhi ya vituo vya kutolea huduma za afya binafsi na tulichobaini ni kwamba majibu ya ugonjwa wa malaria na baadhi ya magonjwa yanatolewa kama njugu ya uongo...sasa hii ni hatari tunatoa onyo kwa vituo hivi kuacha tabia hii sheria itachukua mkondo wake," alisisitiza Dk. Nyembea.

Alisema serikali ina imani kubwa na vituo binafsi vya afya hasa katika kutoa huduma hizo kwa ufanisi, vituo vichache visichafue vingine.

Naye Meneja wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) Mkoa wa Mtwara, Dk. Adofu Kahamba, alisema vituo vya afya ambavyo ni wanachama wa mfuko wa bima ya afya vinapaswa kufanya kazi zao kwa uaminifu na uadilifu vinapotoa huduma kwa wananchi.

Alisema vituo vyote binafsi vinavyotoa huduma kupitia bima ya afya vifanye kazi kwa kufuatia kanuni za taratibu katika kuwahudumia wananchi na wanapofanya vipimo watoe majibu ya vipimo hivyo kwa usahihi unaotakiwa.

Dk. Kahamba alisema iwapo watapata taarifa kituo chochote cha afya mwanachama wa NHIF kubainika kutoa vipimo visivyo sahihi, kitafutwa uanachama wa bima hiyo.

# Uboreshaji miundombinu Bandari Mtwara wakamilika

SERIKALI imekamilisha uboreshaji wa miundombinu ya Bandari ya Mtwara na ununuzi wa vifaa vipya ambavyo vinatarajiwa kuwasili nchini Agosti, mwaka huu.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, alibainisha hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Tunza Malapo.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Bandari ya Mtwara inatumika.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kasekenya, alisema serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), inatekeleza Mpango Mkakati wa miaka mitano (2021/22 - 2025/26), unaolenga kuboresha bandari zote za Tanzania ikiwamo Bandari ya Mtwara.

"Kupitia mkakati huo serikali imekamilisha uboreshaji wa miundombinu ya bandari na ununuzi wa vifaa vipya (Reach stacker, Mobile Harbour Crane, Terminal Tractors) na Ship To Shore Gantry Crane (SSG) ambayo inatarajia kuwasili nchini mwezi Agosti 2022 kwa ajili ya Bandari ya Mtwara," alisema.

Vilevile, alisema serikali kupitia TPA imeendelea kutangaza bandari hiyo ili kuvutia shehena kutoka ukanda wote wa maendeleo wa Mtwara (Mtwara Development Corridor), unaojumuisha nchi tano za Msumbiji, Malawi, Zambia, DRC na visiwa vya Comoro. Alisema, serikali kupitia TPA imepunguza tozo za Bandari ya Mtwara kwa asilimia 30 kuanzia Julai, 2021.

Katika swali lake la nyongeza, mbunge huyo alisema moja ya sababu zinazochangia Bandari ya Mtwara isifanye vizuri ni ukosefu wa meli na makontena ya kusafirishia bidhaa.

"Je, serikali imejipanga vipi kuhakikisha meli na makontena yanafika kwa kuwa huko nyuma zilikuwa zinafika, naomba pia kujua katika msimu huu wa korosho kwa mwaka 2022/23 korosho zitapita Bandari ya Mtwara," alihoji.

Akijibu maswali hayo Kasekenya alisema, kumekuwapo na jitihada za makusudi kwa ajili ya bandari hiyo ikiwamo kupunguza tozo zote kwa asilimia 30 na serikali imeondoa gharama za utunzaji makasha ya kubebea korosho katika msimu mzima uliopita na wa mwaka huu ili kuvutia wafanyabiashara na wenye meli kutumia bandari hiyo.

Alisema kwa msimu wa mwaka huu bandari hiyo ipo tayari kupitisha korosho na kuvutia matumizi ya bandari hiyo.



Mbunge wa Handeni Mjini, Reuben Kwagilwa, akiuliza swali bungeni katika mkutano wa saba kikao cha 48 jijini Dodoma jana, kuhusu serikali kuipatia Hospitali ya Handeni gari la kubebea wagonjwa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mikakati kukabili ugonjwa mnyauko migomba yatajwa

NAIBU Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, ametaja mikakati mbalimbali inayochukuliwa na serikali kukabiliana na ugonjwa wa mnyauko wa migomba mkoani Kigoma.

Mavunde aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kigoma Kaskazini (CCM), Assa Makanika.

Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi wa Kigoma vijijini kukabiliana na ugonjwa wa mnyauko unaoharibu migomba na kuikausha.

Mavunde alisema katika kukabiliana na ugonjwa wa mnyauko wa migomba, serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwamo kutoa mafunzo ya utambuzi na udhibiti wa ugonjwa huo kwa maofisa ugani.

Alisema hadi Juni, 2022 mafunzo kwa maofisa ugani 76 wa Halmashauri ya Buhigwe yametolewa na wamefundisha wakulima mbinu za udhibiti ikiwamo matumizi ya miche bora ya migomba yenye ukinzani wa ugonjwa huo ambayo ni (TALIBAN1, TALIBAN2, TALIBAN3, TALIBAN4, FHIA 23, WILLIAM5).

"Hadi sasa tayari wakulima wamepatiwa miche bora 100 ili kuanza uzalishaji wa miche bora ya kupanda mashambani na kazi hiyo ni endelevu.

Kadhalika, alisema wakulima wameshauriwa kung'oa migomba yote iliyoathirika na Banana Xanthomonas Wilt - BXW.

Alisema wanaendelea kusimamia sheria ya karantini kwa Mkoa wa Kigoma na maeneo mengine nchini ili kuzuia kusambaa kwa ugonjwa huo.

## Taasisi 81 zabainika kutotenga fedha ununuzi 30%

BUNGE limeelezwa kuwa taasisi 81 zilizofanyiwa tathmini na Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA) zimebainika hazijatenga fedha za ununuzi asilimia 30 kwa ajili ya makundi maalumu kwa mwaka 2020/21.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mwanaisha Ulenge.

Mbunge huyo alihoji lini serikali itafanya tathmini kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi wa Umma ya Mwaka 2013 katika Sehemu ya 64(2)(C) ya Kanuni ya 30C kama ilivyofanyiwa marekebisho.

Chande alijibu kuwa matokeo ya tathmini ya mwaka 2020/21 yameonyesha kati ya taasisi 86 zilizofanyiwa ukaguzi, mbili zilitenga fedha hizo, tatu zilitenga kiwango pungufu na 81 hazikutenga kabisa.

kutokana na matokeo hayo, alisema serikali imezielekeza taasisi nunuzi zote kuzingatia matakwa ya sheria na umuhimu wake katika kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Pia, aliagiza vitengo vya ukaguzi wa ndani kuhakikisha kuwa ripoti za kila robo mwaka ambazo huwasilishwa PPRA kuwa na taarifa kuhusu utekelezaji wa sheria katika eneo hilo.


Awali, alisema katika kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 pamoja na kanuni zake, PPRA hufanya tathmini ya ununuzi na kuchapisha taarifa ya tathmini hiyo kila mwaka.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Zaytun Swai, alisema sheria hiyo inataka asilimia 30 ya manunuzi itenge kwa ajili ya makundi maalum ya wanawake na vijana na kuhoji serikali kwanini isitoe maelekezo kwa maofisa masuhuli kuzingatia sheria hiyo.

Naibu Waziri Chande alisema serikali imekuwa ikitoa maelekezo kwa maofisa manunuzi na kuwaagiza kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa.




Habari zote: Augusta Njoji , DODOMA



Ukurasa 14

KADA DK. LAWRENCE GAMA

**Kada anayebaki kioo cha Taifa, nyumbani Ruvuma**



Ukurasa 13

SIKU 48 UCHAGUZI KENYA

Ni Raila pekee na ilani, aahidi kung'oa ufisadi


# siasa

JUMATANO JUNI 22, 2022

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe





Ukurasa 12

**Loliondo jukumu linalohitaji mseto wa mbinu kulitatua**

# Lt. Kanali mstaafu Gangisa; Swahiba, 'class mate' wake Idi Amin jeshini

- Darasani, chumbani wote; kambini pamoja
- Hata walipotengana, mawasiliano palepale
- Yukoje? Alipenda sana vyeo na masumbwi
- Kumsikia kavamia, ghafla akamgeuza adui
- Samora? Swahiba mpya wa harakati uhuru

**Na Gideon Mwakanosya ,**

**SONGEA**

UKIMWONA ni babu hasa kwa leo, umri wake ana miaka 100 kasoro minne. Kitaifa ana upekee unaompa sifa na umaarufu. Ila kijeshi yuko hai kweli kweli, pia amekuwa swahiba hasa wa aliyekuwa Rais wa Uganda Field Marshal Iddi Amin Dada.

Huyo ni Luteni Kanali Mstaafu Daniel Gangisa, aliyeanza utumishi huo katika zama za ukoloni, Umoja wa Mataifa (UN) ukiwa 'mbichi' na ukoloni umemea kila kona ya Afrika, isipokuwa Afrika Kusini zama hizo, nako kukiwapo kiulizo cha uhalali wake, anayesimulia kumjua Amin 'nje na ndani'.

Pia, anadokeza msimamo wake, alipomkera, akautupa uswahiba pipani na kubeba kiapo cha uzalendo akawa mstari wa mbele vitani akichangia mengi kumtokomeza katika vita vya Tanzania na Uganda, mwaka 1978.

Maisha yake yote kufungamana na jeshi, hadi yu babu kamili, lakini hapendi kutengana na jeshi japo kwa 'harufu', akiwa mkazi wa eneo la Chandarua, jirani kabisa na iliko ngome ya Brigedi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), mjini Songea.

Hapo anaiambia Nipashe katika mazungumzo yao mjini hapa hivi karibuni kwamba, maisha yote anajivuna na kuhusudu utumishi wake jeshini, akipatiwa heshima na urafiki wa kudumu na taasisi hiyo.

Nipashe iliyomshuhudia katika makazi hayo akiwa na wake wawili, pia wajukuu kadhaa anajivuna kwamba moja ya heshima anayaoifurahia ni namna wakati wote wanampa heshima kumwalika katika shughuli za kijeshi mahali hapo.



Luteni Kanali Mstaafu Daniel Gangisa (96), wa kushoto na rafiki yake, marehemu Iddi Amin. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## URAFIKI NA AMIN

Luteni Kanali Mstaafu Gangisa, ambaye wajihi wa kijeshi haujamtoka, ni mzaliwa wa mwaka 1927 katika eneo la Ruhuwiko mjini Songea. Akiwa na umri wa miaka 20, alipojiunga na utumishi wa jeshi la wakoloni.

Anasema mwaka 1947 katika zama hizo za ukoloni wa Kiingereza, Gangisa alipelekwa mafunzoni katika Chuo cha Jeshi Nakuru, nchini Kenya mwaka 1953, akisimulia hapo ndio ukawa mwanzo wake wa uswahiba na Iddi Amin na walishibana mno, wote wakiwa vijana ndani ya darasa moja kwa miaka mitatu

"Nimesoma na Idd Amini miaka mitatu kuanzia 1953 hadi 1955, alikuwa rafiki yangu sana! Tena tulilala chumba kimoja bwenini na baada ya kumaliza kozi mimi na Amini tulipata alama za juu, hivyo chuo kilitupa mkataba wa kuwa walimu. Tulifanya kazi sote tukiwa na cheo cha Sajini kwa miaka mitatu," anakumbusha Luteni Kanali Gangisa.

## ALICHOMSOMA KITABIA

Hata hivyo, Gangisa anasema licha ya Amin katika kipindi hicho kuonekana kuwa ni kijana mtulivu na ambaye hakupenda ugomvi, anamfafanua: "Alikuwa mpiganaji wa ngumi na aliniomba anifundishe ngumi, lakini nilikataa."

Afande Mstaafu Gangisa, anafafanua kwa muda aliyoishi na swahiba wake huyo aligundua dosari kubwa aliyokuwa nayo tangu kipindi hicho, muda wote alitamani na kupenda sana vyeo kazini. Anasisitiza "niliposikia ameipindua nchi, sikushangaa kwa sababu nilimfahamu."

Itakumbukwa, Iddi Amin, baada ya kutwaa madaraka ya nchi yake kwa mapinduzi mwaka 1971, alijiongeza cheo cha juu kabisa kijeshi cha Field Marshal, kutoka Meja Jenerali.

Luteni Kanali Gangisa anasimulia, baada ya kumaliza mkataba wa kufundisha Nakuru alirudi eneo la Nyeri nchini Kenya kwenye kambi yake, kutumikia jeshi la kikoloni.

Anasimulia kuna wakati walipelekwa wote kwenda kupigana Mauritius, akiwa na swahiba huyo Amin na baada ya kurejea kutoka Mauritius, Amin alirudi kwao akimwacha yeye Kenya.

Mzee Gangisa anasimulia, wakati huo moja ya wajibu mkubwa wa jeshi la kikoloni wakati huo, ilikuwa kukabiliana na harakati za uhuru za Kenya, Mauamau.

Ni lini mara ya mwisho kuonana na Iddi Amin? Swali hilo aliloulizwa na Nipashe, Luteni Kanali Gangisa analifafanua kwamba, ilikuwa mwaka 1960 ingawaje waliendelea kuwasiliana kwa miaka mingi baadaye.

Anarejea, hata Mwalimu Julius Nyerere alipoanza harakati zake za kuunda chama cha TANU nchini Tanganyika mwaka 1954, Mzee Gangisa anasimulia walikuwa wameshikamana kirafiki na Amin, chuoni Nakuru, Kenya.

"Idd Amin ndiye aliyenipa taarifa kwamba 'wewe Mswahili', nyumbani kwako kuna bwana (Nyerere) ameanzisha chama (TANU) cha kupigania uhuru. Alinitisha 'Maumau itahamia kwenu.' Nikamwambia 'Mungu yupo!' Alikuwa anaongea Kiswahili kizuri, alikuwa rafiki yangu mkubwa sana,' anakumbusha Afande Gangisa.

Kimsingi, nyendo za kusaka uhuru wa Maumau, ziliendana na mapambano ya silaha kusaka uhuru wa Kenya, uliopatikana mwaka 1963, ukitanguliwa na Uganda mwaka 1962.

## ALIVYORUDI NYUMBANI

Luteni Kanali Mstaafu Gangisa, anaisimulia Nipashe kwamba, wakati alikuwa Kenya wanaharakati wa Mauamau walitaka kujenga naye uswahiba wa siri, ili awe mamluki wao akiwa ndani ya jeshi la kikoloni.

Anasema, ni mkakati aliouona unampa mtihani hata akaukwepa kwa kuomba asipewe mkataba zaidi kutumika nchini Kenya, akitaka arejeshwe nyumbani Tanganyika kuendelea na


**INAENDELEA UK. 13**

# Loliondo, jukumu linalohitaji mseto wa mbinu kulitatua

• Kuelewesha, kuwahamisha wananchi kuhama




Kazi ya kuwahamisha wenyeji kutoka Loliondo. **PICHA: MTANDAO**

**Na Nimi Mweta**

VURUGU zinazotokana na maamuzi ya kuhama na kupisha utunzaji endelevu wa hifadhi ya Ngorongoro katika wilaya ya Loliondo mkoani Arusha ni mtihani mwingine wa kiutawala ambao sasa unausumbua uongozi wa taifa.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, amefika huko mara kadhaa kusimamia mazungumzo na serikali ili wananchi waelewe kinachotokea, na kinachohitaji kufanyika, na kwa kiasi fulani amefaulu kufikisha ujumbe.

Hata hivyo , upinzani uliojikita katika jadi na dhana ya wanamazingira kuwa wakazi wa jadi hawaharibu mazingira, una ushawishi mkubwa.

Ikafikia mahali bunge linaahirisha majadiliano yake ya kawaida na kuangalia hali ilivyo Loliondo, kukawa na vurugu hadi kuuawa polisi , hivyo ikamlazimu Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Simon Sirro, kwenda kukagua eneo hilo kwani limekuwa uwanja wa mapambano .

Ni kama vile kunahitajiwa kanda maalum ya polisi, endapo ulinzi na usalama kwa hali ya kawaida unaanza kuwa wa mashaka.

> Kuna msemo wa Kiswahili kuwa 'penye udhia, penyeza rupia,' kwani rupia inayeyusha udhia wote, mtu akijisikia 'hajambo' kwa pesa aliyopata.

Mwelekeo serikalini unakuwa ni kuufuatilia 'mkono uliojificha' katika vurugu hizo, kwani huenda yapo makundi ya wadau wa nje na ndani ya nchi wasioridhika na sera hiyo.

Hadi hivi karibuni bado baadhi ya wadau hao wamekuwa wakitoa matamshi ya nguvu kuhusu suala hilo, wakati mmoja zikaja taarifa kuwa wapo wazee waliozungumza katika mkutano wa hadhara kuwa wananchi hawataondoka, tena wako tayari kupigania kuondolewa sera hiyo, yaani kuwaondoa katika ardhi yao ya jadi.

Ni moja ya maeneo ambayo yanahitaji elimu kwa kiasi fulani, ila siyo ili mtu aelewe aache mwelekeo alio nao, ila kama utangulizi wa kuelewa msingi wa hatua ya pili ambayo inalenga maslahi, kuwa iwe inakubalika na kuvumilika, na hata kuleta matamanio kwao.

Akiwa Loliondo hivi karibuni, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, anasema kuna makundi ya watu ambayo yanatumika kuchochea na kuwasha moto wa kutoelewana kati ya serikali na wananchi, jambo analosema halikubaliki.

Hayo yanatokea baada ya Spika Dk Tulia Ackson, kuitaka serikali kueleza kilichomo katika video mitandaoni ya wakazi wa Loliondo wakiwa wameshika sime kutishia amani, wakipinga kuondolewa huko.

Anachosisitiza Waziri Mkuu ni kuwa hakuna mtu atakayelazimishwa kuhama, maelezo ambayo ni sehemu ya elimu au taarifa ya kina inayotangulizwa na serikali, zaidi kuhusu uhifadhi.

Kilichosababisha vurugu ilikuwa ni mwendelezo wa zoezi la kupiga ramani eneo hilo kwa kuweka mawe ya kisanifu kuonyesha ni wapi na kituo gani katika mpaka wa eneo husika linalopimwa.

Ni wakati ambao zoezi la kuwahamisha wakazi wa vijiji 14 vinavyozunguka eneo maalum la mapito ya wanyama na kinachoonekana ni kuwa wakazi hao wamebaki na umoja wao licha ya baadhi yao kukubali kuhamia Handeni, ambako serikali inatayarisha makazi bora, huduma jamii, eka tatu za ardhi ya kaya na eneo pana la malisho ya pamoja ya ng'ombe.

Kwa kuwa mwelekeo huo ni wa kuwahamisha kama kundi, wale wasiotaka kuhama kwa udi na uvumba wanazungumza kwa kujiamini, kwa sababu suala hilo bado ni la kundi, si la maamuzi ya mtu mmoja mmoja.

Kwa maana hiyo, zinahitajiwa mbinu tofauti za kuchanganya 'karoti'na 'fimbo' kama inavyoitwa katika fasihi, kwani 'fimbo' pekee zitaleta ugomvi mkubwa kati ya wananchi na serikali, ila 'karoti' zinazotolewa kwa jamii hiyo kwa pamoja zinaulinda umoja wao wa kijamii, kuwezesha uchochezi kujikita miongoni mwao.

'Fimbo' inayoweza kutumika bila madhara ni kukumbushana kuwa ardhi yote ni mali ya pamoja ya wananchi wa Tanzania, na serikali ndiyo yenye dhamana ya matumizi yake; kuwa hii ndiyo maana ya kuwa nchi, kuwa makabila hayana 'haki isiyohamishika' ya umiliki ardhi.

Hilo likishaeleweka, serikali itoe amri nyingine ya 'karoti,' kununua ng'ombe wote walioko pale kwa bei mara tatu ya soko, watwae, ndipo wahame.

Umuhimu wa mpango huo ni kuiyeyusha jadi ambayo inakinzana na mpango wa kuhamia katika nyumba zilizojengwa kimjini.

Hata kama kuna ardhi kubwa, na kwa maana hiyo kuna haja ya kutoa nafasi ya kila mmoja wao kupanga ni maisha gani anataka, ili mradi asiwe anafuga ng'ombe hapo Loliondo. Ili afanye maamuzi kama hayo kwa uhuru inabidi 'kumfidia kwa kumjaza mapesa' kama alivyowahi kusema John Cheyo, kiongozi wa UDP.

Kuna msemo wa Kiswahili kuwa 'penye udhia, penyeza rupia,' kwani rupia inayeyusha udhia wote, mtu akijisikia 'hajambo' kwa pesa aliyopata.

Ni moja ya vielelezo vya mitaala ya maumbile, kuwa 'nguvu kuu' ya kisaikolojia katika maisha ni maslahi binafsi, ila 'nguvu dhaifu,' yaani maslahi ya wengi au ya pamoja, ndiyo inaunganisha watu kimaadili au kisiasa, hivyo jadi isitumike kuvuruga.

Inahitaji kuyeyushwa kwa rupia, ila siyo kwa kuwabembelezea hiyo rupia kwani nafsi itaona aibu; ni pale ambapo kuna mjeledi, 'chukua fidia ya pesa uhame, au uhame bila pesa.'

Baada ya mkakati huo kuwekwa, polisi waweke doria maeneo yote kuzuia watu wasiingize mifugo kutoka nje. Ikumbukwe kuwa kuna fedha nyingi katika mifuko ya kimataifa ya kulinda mazingira kwa jumla na hata hifadhi, hivyo 'biashara' kama hiyo haihitaji kuwa mzigo kwa serikali ishirikishe wadau wengine pia.

## Lt. Kanali mstaafu Gangisa; Swahiba, 'class mate' wake Idi Amin jeshini

**INATOKA UK. 11**

utumishi wake wa kijeshi la Kikoloni, akakubaliwa.

Bila ya kuingia na mada hiyo kwa kina, anasema alipokuwa katika utumishi huo wa jeshi nyumbani Tanganyika, akampa ushirikiano Mwalimu Nyerere na harakati zake za uhuru wa TANU, hata nchi ilipopata uhuru mwaka 1961, aliendelea na utumishi wa jeshi.

Anajitambulisha kuwa alishiriki mwaka 1964 katika kuunda JWTZ, yeye akiwa ofisa wa 50 wakati huo, akiwa na cheo cha Luteni Kanali.

**AMREJESHEA AMIN KIPIGO**

Luteni Kanali Mstaafu Gangisa anasema, alistaafu kazi ya JWTZ mwaka 1978, lakini baada ya kusikia rafiki yake Amin aliyeipindua Serikali ya Uganda, sasa kauvamia Mkoa wa Ziwa Magharibi (sasa Kagera), aliamua kuahirisha kustaafu, akaomba kurudi kazini kupambana na rafiki aliyegeuka adui yake.

"Nilisema kama amevamia nchi yetu, ninarudi jeshini! Tulipambana naye, nilifika hadi kijijini kwake, na makao yake Kampala pale alinusurika kuuawa, akatorokea njia ya Kenya. Tuliwaomba Kenya wafunge mpaka, walikataa, hivyo Iddi Amin akanusurika, akatoroka ukiwa ndiyo mwisho wa vita vya Uganda," anasimulia.

Vita vya Tanzania na Uganda, maarufu Vita vya Kagera, vilipiganwa kuanzia Oktoba 30 mwaka 1978 hadi Aprili 11, 1979 vilipomalizika.

Luteni Kanali Gangisa anaeleza uzoefu wake mwingine ni kushiriki harakati na Rais wa Msumbiji na kiongozi wao, Samora Machel, akikumbuka mara kadhaa amelala pamoja naye kwenye mahandaki.


Anasimulia kumbukumbu yake, Samora alivyofika Songea baada ya Uhuru wa Msumbiji mwaka 1975, akamshukuru Luteni Kanali Gangisa kwa upekee. Katika hotuba yake kwa umma, akimnukuu kauli yake kwamba, amempa ushirikiano wa kumpatia silaha na walilala wote kwenye mahandaki na walikula mihogo ya wenyeji, wakati wa mapambano dhidi ya ukoloni wa Kireno.

Ni kwa muda mrefu wa harakati za ukombozi Msumbiji, Samora akiwa mpiganaji aliyeivishwa, walikuwa na mgome zao mkoani Ruvuma, Lindi na Mtwara, hasa katika wilaya kama Tunduru na Nachingwea.

SIKU 48 ZA UCHAGUZI KENYA



David Mwaure Waihiga, ingizo jipya kwenye uchaguzi mkuu wa urais wa Kenya. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Rastafariani George Wajackoyah ni miongoni mwa watakaochuana kwenye urais wa Agosti 9, 2022.

# Ni Raila pekee na ilani, aahidi kung'oa ufisadi

• Ruto na sera ya kujaza masikini pesa

**Na Mwandishi Wetu**

Ni mchuano unaowahusu wanaume wanne wapo wapinzani wakuu Raila Odinga na Naibu Rais William Ruto, ambao Agosti 9, Wakenya watapiga kura kumchagua nani kati yao awe rais.

Kwa sasa, kuna wagombea wanne wanaowania kumrithi Rais Uhuru Kenyatta, ambaye kikatiba hawezi kuendelea na wadhifa huo baada ya kukaa ikulu kwa mihula miwili ya miaka mitano.

Juni 6 mwaka huu , Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ya Majimbo (IBEC) ilihitimisha mchakato wake wa uhakiki na kupunguza idadi ya washiriki kutoka 55 hadi wanne. Baadhi ya walioenguliwa ni pamoja na mgombeaji binafsi Jeremiah Nyagah.

Hatua hiyo inawabakiza kwenye kinyang'anyiro wapinzani wawili wakuu wanaosalia kuwa wagombea tishio kinara wa upinzani Raila Odinga, ambaye Rais Kenyatta ametangaza hadharani kuwa anamuunga mkono mia kwa mia , na William Ruto, Naibu Rais, anayetoka kivyake.

Raila Odinga ana historia akianzia Orange Democratic Movement, wakati huo aligombea urais wa Kenya kwa mara ya kwanza mwaka 1997 na kuibuka mshindi wa tatu.

Katika mchuano wa mwaka huu, Raila ana jaribu tena kwa mara ya tano.

Odinga, mmoja wa wanasiasa maarufu nchini Kenya, ni mgombea anayetoka katika ukoo ulioanza harakati za uhuru wa Kenya mhusika mkuu akiwa baba yake Jaramogi Oginga Odinga, shujaa wa uhuru na Makamu wa Kwanza wa Ris wa Kenya.

Jaramogi alikuwa rafiki na mgombea mwenza wa Jomo Kenyatta, babake Uhuru, na rais wa kwanza wa Kenya.

Raila akiwa na miaka 77 amewahi kuwa Waziri Mkuu wa Kenya kati ya mwaka 2008 na 2013 wakati huu Rais Mwai Kibaki (marehemu) akiliongoza taifa katika muungano mkuu ambao uliundwa baada ya mazungumzo ya amani yaliyosimamiwa na aliyekuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Kofi Annan (marehemu).

Ni katika uchaguzi ambao matokeo yake yalileta mtafaruku mkubwa mwaka 2007 ambao Kibaki alishinda na Odinga akashika nafasi ya pili jambo ambalo hakulikubali. Kulizuka vurumai nyingi zilizosababisha umwagaji damu mkubwa katika maeneo mengi ya Kenya.

Mara nyingine tena Odinga alishindwa katika uchaguzi wa mwaka 2013 na 2017 pia na Uhuru Kenyatta. Hata hivyo, juhudi za maridhiano leo zimesababisha Rais Uhuru kumuidhinisha mpinzani wake Odinga kuwa mgombea anayeungwa mkono na serikali.

Wakati huo huo, Raila Odinga, amemchagua Martha Karua, Waziri wa Sheria wakati wa awamu ya Kibaki, kama mgombea mwenza wake ili kushawishi na kupata kura nyingi kutoka kwa Wakikuyu, kabila kubwa zaidi nchini humo na lenye kura na nguvu nyingi za kisiasa.

**MBIU YA UCHAGUZI**

Kaulimbiu ya kampeni ya Odinga ni kukabiliana na ufisadi na kurekebisha mianya ambayo anasema inawanyima Wakenya huduma za kimsingi. Pia anaahidi maridhiano ya kitaifa ili kuunganisha nchi, mageuzi kwenye sheria na mahakama pamoja na ustawi wa jamii hasa kwa Wakenya kutoka kaya maskini.

Ndiye mgombea pekee wa urais ambaye amezindua rasmi ilani ya uchaguzi au manifesto akieleza kile anacholenga.

> "Ruto mwenye miaka 55 sasa anakabiliwa na vita kali ya kupambana na Odinga anayeungwa mkono na Kenyatta katika azma yake ya kuwa rais tena baada ya kugombea kwa miaka mitano.

**MGOMBEA RUTO**

William Ruto Makamu wa Rais anagombea toka chama cha The United Democratic Party. Kijana huyu shujaa licha ya kupingwa na kuzodolewa na ikulu ya Kenyatta, yuko vizuri na anapambana.

Ruto aliyejulikana kwa mara ya kwanza mwaka wa 1992 baada ya kusaidia kupatikana kwa kikundi maarufu cha ushawishi cha Youth for KANU 92 (YK92), ambacho kilisaidia chama tawala cha Kenya African National Union kubaki madarakani, ameamua kushindana.

Amekuwa mbunge kwa miaka kadhaa kisha akawa waziri katika wizara mbalimbali kwa miaka kadhaa hadi 2007. Ulipofika wakati huo wana KANU wengi na vigogo wakiwamo Raila, walikuwa wamejiondoa katika chama tawala cha KANU baada ya rais Mwai Kibaki kumteua Kenyatta kumrithi.

Ruto alichaguliwa pamoja na Rais Uhuru kuongoza taifa na tangu wakati huo kumekuwa na madai na kashfa za kila kambi kati ya Ruto na Kenyatta kukashifiana.

Uhuru anadai Ruto ni fisadi na mwenye uchu wa mamlaka na madaraka makuu lakini Ruto naye anadai Ikulu ya Kenyatta na washirika wake walipanga njama ya kumuangamiza.

**KESI YA ICC**

Mwaka 2010, Ruto alishtakiwa na Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) mnamo Desemba 2010 kwa mashtaka kadhaa ikiwa ni pamoja na mauaji wakati wa ghasia zilizotokea baada ya uchaguzi wa 2007.

Wengi walidhani kuwa huo ungekuwa mwanzo wa mwisho wa kazi yake kisiasa, lakini badala yake, aliteuliwa kuwa mgombea mwenza na Makamu wa Rais .

Wakati Uhuru alipoachilia kiti chake kwa muda ili kujibu mashtaka katika mahakama ya ICC ambayo pia Ruto alihusika, hata hivyo yalitupiliwa mbali baadaye wakaendelea kuwa viongozi wakuu wa nchi.

Ruto mwenye miaka 55 sasa anakabiliwa na vita kali ya kupambana na Odinga anayeungwa mkono na Kenyatta katika azma yake ya kuwa rais tena baada ya kugombea kwa miaka mitano.

Mgombea mwenza wa Ruto ni Rigathi Gachagua kutoka Mlima Kenya na mkosoaji mkubwa wa Rais Kenyatta.

**MBIU YA KAMPENI**

Ruto ameelekeza kampeni yake katika kuunda mpango mpya wa uchumi wa chini kwenda juu, ambao anasema utawajaza Wakenya mapesa kwenye mifuko hasa watu wa kawaida.

Kambi yake inaahidi Shilingi bilioni 50 za Kenya (Dola milioni 425) zikilenga biashara ndogo ambazo ni kichocheo kinachohitajika ili kuwainua wenye kipato cha chini kutoka kwenye umaskini.

**DAVID WAIHIGA**

Mgombea Waihiga anatoka katika chama cha Agano Party. Tofauti na Raila na Ruto, David Mwaure Waihiga si jina maarufu katika ulingo wa siasa za Kenya ingawa amekuwa akijihusisha na siasa kwa zaidi ya miaka 12 sasa.

Ni wakili mzoefu wa zaidi ya miaka 35, alianza mikiki kwenye uchaguzi wa 2013 chini ya chama hicho, hata hivyo, alijiondoa katika kinyang'anyiro cha kuwania ugavana wa Kaunti ya Lamu katika pwani ya Kenya.

Waihiga anaamini kwamba serikali inahitaji damu mpya kushughulikia matatizo mengi ya Kenya na anatarajia kuleta mambo mapya licha ya uchanga wake kisiasa .

**GEORGE WAJACKOYAH**

George Wajackoyah, ni mgombea wa nne anatoka katika chama cha Roots Party, naye ni wakili mzoefu mwenye digrii tano, anajulikana kwa mijadala na matamshi yake ya kisiasa yenye utata.

Kiongozi huyo wa chama cha Roots mwenye miaka 61 analeta sifa za 'rastafarian' kuhalalisha bangi, ambayo anasema itasaidia kumaliza madeni makubwa ambayo Kenya inadaiwa.

Wajackoyah, profesa wa sheria na mtumishi wa kitengo cha intelijensia, anatetea ufugaji wa nyoka na kuongeza siku za kupumzika ziwe tatu badala ya mbili. **MITANDAO**

JUKWAA LA VIONGOZI

KADA DK. LAWRENCE GAMA



Timu ya soka ya Majimaji na Uwanja wa Majimaji, vyote ni zao la Dk.Lawrence Gama, alipokuwa Mkuu wa Mkoa Ruvuma. **PICHA ZOTE: GIDEON MWAKANONSYA**

# Kada anayebaki kioo cha Taifa, nyumbani Ruvuma

**Na Gideon Mwakanosya,**

SONGEA

HIVI sasa imetimu miaka 14 nchi ikimkosa jina lake maarufu, Dk. Lawrence Gama, mwenye sifa ya kuwa kada kindakindaki wa itikidi na siasa za kitaifa, Ujamaa na Kujitegemea.

Pia, msomi huyo, yumo katika orodha ya waasisi wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), hata akadumu katika safu ya vijana watiifu wa uongozi wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, serikalini na ndani ya chama, TANU hadi CCM.

Lakini, unaporejea kwa 'wana-Lizombe' daima amepatunza nyumbani Ruvuma mkoa alikozaliwa kwa mengi, akipahusudu kupindukia.


Yanapotajwa machache, nyayo zake zinaonekana kwenye msukumo wa ukombozi wa ujenzi wa Barabara ya Makambako hadi Masasi, iliyoengua kwenye madhila ya Mlima Lukumburu, wana-Ruvuma wakishuhudia kuzinduliwa barabara mpya iliyoikwepa milima hiyo chini ya kampuni ya Balfour Beatty.

Lingine, mkoa wa Ruvuma ulitamba sana na klabu ya soka ya Majimaji, ufanisi usiohitaji ufafanuzi, mkoa huo kuwa katika iliyopewa jina la 'the big four' kwa maana ya wazalishaji wakubwa wa nafaka mahindi kitaifa.

Ndani ya ufafanuzi huo, Dk. Gama bado anaishi akijumuishwa kwa wasifu; kada aliyeiva na kuwa msaada mkubwa kitaifa , mlinzi wa usalama wa nchi, kiongozi na mwana- Ruvuma ambaye 'humwambii kitu'.

Ndani ya Chama Cha Mapinduzi, huyu ndiye Mtendaji Mkuu, aliyeshikilia usukani wa CCM kuvuka kutoka zama za uchaguzi

> Mwaka 1989 aliteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora anakokumbukwa kwa kujenga Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi wakati a 1993 alipewa jukumu la kuwa Katibu Mkuu wa CCM.



Marehemu Dk. Lawrence Gama.

wa chama kimoja cha siasa hadi vyama vingi mwaka 1995.

**ANAVYOENDELEA KUISHI**

Dokta Gama anaendelea kuishi mkoani Ruvuma na Tanzania kutokana na kuacha kumbukumbu nyingi ambazo baadhi ya wananchi wanamtaja kuwa ni kiongozi ambaye ameiweka Tanzania na Ruvuma juu kisiasa, kiuchumi na kimaendeleo kwenye nyanja nyingi.

Kitaifa Gama anakumbukwa kwa kuwa kati ya maofisa wachache walioasisi JKT na baadaye kuteuliwa kuwa Mkurugenzi wa jeshi hilo, kisha akapewa wadhifa wa Mkurugenzi wa Idara ya Usalama wa Taifa.

Mkoani Ruvuma, leo wanamkumbuka Dk.Gama kwa yao, wakitaja baadhi kuwa ni mtindo wa kuunganisha nguvu za pamoja, kuthamini utu, uhusiano kazini na kupinga rushwa.

Inaelezwa, kuwa alipoteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kuanzia mwaka 1977 hadi 1987, ndiyo akaanzisha kilichoitwa 'Agizo la Mlale' ambalo kimsingi lilikuwa kichocheo cha kusukuma maendeleo ya Mkoa wa Ruvuma.

Hapo zaidi, lilijikita katika kilimo cha kisasa, kujenga nyumba bora za tofali za kuchoma na kuezekwa kwa mabati, ushuhuda wa kiserikali ukiwa ni ujenzi wa uwanja wa Majimaji.

Uwanja huo ukatafutiwa pacha wake wa kuanzishwa Klabu ya Soka ya Majimaji iliyochukua ubingwa wa Tanzania mara mbili, iking'ara na wachezaji wake maarufu kama Celstine Sikinde Mbunga na Mhando Mdeve.

Mwanamapinduzi Lawrence Gama, akiwa kwenye uongozi wake mkoani Ruvuma hakukubali njaa, akasimamia ubunifu wa Kampeni ya Kuondoa Njaa Tunduru ikijulikana zaidi kama KUNJATU, pale wilaya hiyo ilipokumbwa na uhaba wa chakula.

Lingine linaliongia kwenye historia yake, ni kubuni na kusimamia ujenzi wa Makumbusho ya Mashujaa wa Majimaji, mwaka 1980, eneo la Mahenge mjini Songea. Tangu mwaka 2010 yamepandishwa hadhi na kuwa Makumbusho ya Taifa ya Majimaji.

Pia, kuna Soko Kuu la Songea, baada ya soko la zamani kuungua.

**SAFARI YAKE**

Kada huyo,alizaliwa Januari 19, 1935 katika Kijiji cha Chiulungi Peramiho (sasa wilaya) wilayani Songea mkoa wa Ruvuma, akiwa mtoto wa pili kwa Baba yake Nduna Adam Gama na Mama Veronica Mlangeni.

Alisoma katika Shule za Msingi Magagura na Peramiho darasa la kwanza hadi la nane na kisha kujiunga na Sekondari ya Wavulana Ndanda wilayani Masasi mkoani Mtwara.

Baada ya hapo akapata fursa ya kusoma Cheti cha Sheria katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kisha, akaendelea na masomo zaidi hadi ngazi ya Shahada ya Uzamili ya Siasa na Uchumi katika Chuo Kikuu cha Berlin nchini Ujerumani Mashariki.

Baada ya hapo akaendelea na maudhui hayo ya taaluma kwa ngazi ya shahada ya udaktari (PhD) katika chuo hicho.

Kwa historia ya utumishi wake wa umma, Dk. Gama alipata mafunzo kazini sehemu mbalimbali, yakiwemo ya uofisa wa kijeshi, uongozi wa vijana uliomfikisha Israeli na usalama nchini Uingereza.

Aidha, safari hizo za elimu zilimsogeza hadi Romania na China, Marekani na Ireland.

Mwanasiasa huyu wakati wa uhai wake amewahi kufanya kazi mbalimbali zikiwemo Mkaguzi Msaidizi Idara ya kazi (Labour Inspector), Kamanda wa Polisi Wilaya za Bukoba na Ukerewe.

Historia ya Hayati Gama haiishii hapo inakumbusha kuwa mwaka 1975 aliteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, wakati mwaka 1977 aliuongoza Mkoa wa Ruvuma akitumikia hadi mwaka 1987.

Mwaka 1989 aliteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora anakokumbukwa kwa kujenga Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi wakati a 1993 alipewa jukumu la kuwa Katibu Mkuu wa CCM na mwaka 1995 aliteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro ambapo kuanzia mwaka 1995 hadi mwaka 2005 alichaguliwa kuwa mbunge wa Songea Mjini.

Watanzania wengi kuanzia wanamichezo,wasiasa na majeshi wataendelea kumkumbuka Gama kama kiongozi aliyethamini kazi na michezo.

Akianzisha timu ya Soka ya Milambo FC ya Tabora na Majimaji.

Alifariki Desemba 13, 2008 katika Hospitali ya Aghakhan jijini Dar es Salaam na kuzikwa kijijini kwake Amani Makoro wilayani Mbinga mkoani Ruvuma.

Hakuna ubishi Dk.Lawrence Gama ataendelea kukumbukwa kwa sababu kazi alizosimamia zinaendelea kuishi na kuwanufaisha Watanzania wote.





## Takwimu viwanda usindikaji kusaidia wawekezaji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema ina jukumu la kuhakikisha inakuwa na takwimu sahihi ya viwanda vya usindikaji chakula ili kusaidia kutatua changamoto zinazowakabili wawekezaji wa uchakataji vyakula.

Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Exaud Kigahe, alibainisha hayo juzi wakati wa uzinduzi wa ripoti ya utafiti wa nafaka iliyohusisha viwanda vidogo, kati na vikubwa nchini, chini ya Shirika la Chakula Duniani (WFP).

Kigahe, alisema lengo la serikali ni pamoja na kusimamia ubora wa viwanda nchini kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo nchini (SIDO), ili kusaidia wazalishaji na wasindikaji waendelee kuweka virutubisho kwenye uzalishaji wao.

"Jukumu la serikali ni kuhakikisha inafahamu idadi ya viwanda vilivyopo sababu kubwa ya kufanya hivyo ni pamoja na kulinda usalama wa wananchi kwenye chakula," alisema Kigahe.

Alishauri SIDO kuwatengea maeneo tofauti yenye mazingira mazuri wachakataji wa bidhaa za nafaka ili kuepuka uchafuzi wa mazingira jambo litakalosaidia wazalishe kwa tija na bila usumbufu wa aina yoyote.

Hata hivyo, Kigahe alisema kufanya utambuzi wa viwanda na namna vinavyofanyakazi kutasaidia kupunguza suala la utapiamlo na udumavu katika baadhi ya maeneo kutokana na wasindikaji na wachakataji wa bidhaa kuwa na virutubisho vyote.

"Utambuzi wa idadi ya viwanda ni jambo la muhimu sana kwasababu linasaidia kusimamia uzalishaji na usindikaji unaofanywa kwenye nafaka," alisema Kigahe.

Alisema matokeo ya utafiti yaliyofanywa chini ya usimamizi wa WFP yana umuhimu kwa taifa kutokana na kusaidia serikali kujua kuna viwanda vingapi vya usindikaji nafaka ikiwamo kujua aina za mashine zinazotumika kusindika nafaka.

"Nawapongeza sana WFP kutokana na utafiti uliofanywa hii itasaidia serikali kutatua changamoto zilizoko," alisema Kigahe.

Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Chakula Duniani (WFP), Sarah Gordon Gibson, alisema kabla ya ripoti kutangazwa awali ilifanyika sensa ya kina kuhusu viwanda vya kusaga nafaka nchini ikiwamo kukusanya data zote ili kuelewa maeneo, usambazaji, uwezo na bidhaa zinazosagwa kuhakikisha usalama wa chakula.

Hata hivyo, alisema anaishukuru serikali kutokana na kutoa ushirikiano mkubwa katika suala la upatikanaji data wakati wa utafiti na kuahidi kuendelea kufanya kazi kwa ukaribu zaidi na serikali ili kuhakikisha usalama wa chakula unakuwapo.

# Serikali kubaini maeneo yenye uhitaji watumishi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imesema itashirikiana na Ofisi ya Rais, Utumishi kujua maeneo yenye uhitaji mkubwa wa watumishi ili mabadiliko ya mitaala yanayoendelea yazingatie hilo. Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Francis Michael, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kupokelewa na watumishi wa ofisi hiyo baada ya kuteuliwa na Rais Samia Suluhu hivi karibuni.

Alisema moja ya mikakati yake ni kuendeleza mchakato wa kuboresha mitaala ya elimu na kuimarisha vyuo vya kati ili kuziba pengo la mahitaji ya taaluma na ujuzi yaliyopo.

Alisema wanataka kuangalia kada zipi ambazo serikali inazihitaji ili vyuo vinavyotakiwa kujengwa na mitaala itakayokuwapo ilenge kuziba hilo pengo.

"Najua Wizara ya Utumishi imefanya uchambuzi kujua mapengo gani ya taaluma ambayo yanatakiwa ili kuziba na mitaala inatakiwa kulenga huko," alisema.

Alisema atahakikisha anasaidia kutimiza malengo ya Rais Samia Suluhu Hassan kwenye masuala ya elimu.

"Rais hivi karibuni amezungumza kuhusu masuala ya mapitio ya mitaala mambo hayo ni pamoja na yatakayonilenga mimi ninayopaswa kufanya," alisema.

Alisema wizara ina mkakati wa kuimarisha vyuo vya kati na kuwa tayari serikali imeshasaini mkataba wa kujenga taasisi hizo katika mikoa 15.

Akizungumza na watumishi, Katibu Mkuu huyo aliomba ushirikiano kwa watumishi wa wizara hiyo na kuwataka wasimwangushe.

"Masuala ya watumishi hamtapata shida, lakini usipotekeleza wajibu sitakuwa na mzaha, tufanye kazi kama timu," alisema.




Naibu Meya ya Jiji la Dodoma, Emmanuel Chibango, akifungua mkutano maalumu wa Baraza la Madiwani kwa ajili ya kupitia na kujadili taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) uliofanyika Dodoma jana. Kushoto ni Joseph Mafuru Mkurugenzi wa Jiji na Kaimu Katibu Msaidizi wa Mkoa, Nathalis Limuma. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# H'shauri Dodoma yapata hati safi miaka minne

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imefanikiwa kupata hati safi ya ukaguzi wa hesabu za serikali kwa miaka minne mfululizo baada ya taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kutolewa hivi karibuni.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, alibainisha hayo juzi alipokuwa akiwasilisha taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa hesabu za halmashauri ya Jiji la Dodoma mwaka ulioishia Juni 30, 2021.

Mafuru aliwasilisha taarifa hiyo kwenye mkutano maalum wa Baraza la Madiwani kwa ajili ya kupitia na kujadili taarifa za CAG katika ukumbi wa mikutano wa jiji hilo.

Alisema katika ukaguzi wa hesabu za mwaka 2020/2021, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ametoa hatisafi (unqualified opinion).

"Hati hii inafanya Jiji la Dodoma kuendelea kupata hati safi tangu mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021. Kwa upande wa hesabu za Mfuko wa Afya (busket fund) kwa mwaka 2020/2021, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pia ametoa hati safi (unqualified opinion)," alisema Mafuru.

Akizungumzia hoja za ukaguzi, alisema kuwa taarifa hiyo inaonyesha kuwa halmashauri ina jumla ya hoja 44 kwa mwaka 2020/2021.

"Katika hoja hizo, 16 ni za miaka ya nyuma na 28 ni za mwaka 2020/2021. Mheshimiwa Mwenyekiti hoja zote zimejibiwa na kuwasilishwa kwa mkaguzi wa nje ndani ya siku 21 kama inavyotakiwa kwa mujibu wa sheria.

"Uhakiki wa majibu yaliyowasilishwa kwa mkaguzi yatahakikiwa katika ukaguzi wa mwaka," alisema.



# Wamiliki magari ya wanafunzi waagizwa kuyakarabati

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani mkoani Mbeya, limefanya ukaguzi maalum wa magari ya kusafirisha wanafunzi na kubaini idadi kubwa yana hitilafu zinazoweza kuhatarisha maisha ya watoto hao wakati wowote.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, ACP Meroe Buzema, aliongoza ukaguzi huo juzi na kubaini dosari mbalimbali kwenye magari hayo.

Miongoni mwa dosari hizo ni pamoja na uchakavu wa magari, viti wanavyokalia wanafunzi kutokuwa imara pamoja kutofanyiwa maboresho ya mara kwa mara.

Kamanda Buzema aliagiza wamiliki wa shule kufanya ukarabati wa magari ya kubebea wanafunzi ili kuwaepusha na hatari zinazoweza kugharimu maisha ya watoto.

Aliwaagiza wamiliki wa shule kurekebisha magari hayo ili kujihakikishia usalama wa watoto na atakayekiuka maagizo hayo gari litakamatwa na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria," alisema Buzema.

Baadhi ya madereva wa magari ya shule akiwamo Atupele Lazaro, alilipongeza Jeshi la Polisi kwa kufanya ukaguzi huo hatua itakayosaidia wamiliki wa shule kufanya matengenezo ya magari hayo.

Alisema baadhi ya wamiliki ni wagumu kufanya matengenezo ya magari ya kubebea wanafunzi, hatua hiyo itasaidia kutambua umuhimu wa kuboresha vyombo hivyo.

Katika hatua nyingine, Kamanda Buzema alisema wanamshikilia dereva wa basi la Arusha Express, linalofanya safari zake kati ya miji la Mbeya na Arusha baada ya kufanya ukaguzi wa kushtukiza barabarani na kumkuta akiendesha gari huku akiwa amelewa chakari.

Alisema walimtia nguvu eneo la Chimala wilayani Mbarali baada ya kufanya ukaguzi wa kushtukiza na kwamba kitendo hicho kilikuwa kinahatarisha maisha ya abiria.



Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, jana, akizungumza na wananchi wa Kata ya Nkung'ungu wilayani Chunya, Mkoa wa Mbeya juu ya kilimo cha maharagwe ya soya ambacho kinatarajiwa kuanza baada ya mwekezaji wa ekari 100,000 kupatikana wilayani humo. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Ukosefu chakula kwa wanafunzi chanzo kufanya vibaya

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

UKOSEFU wa chakula cha mchana kwa wanafunzi wa shule za msingi wilayani Mbarali katika Mkoa wa Mbeya, imekuwa sababu ya watoto wengi kushindwa kumudu masomo yao na kuchangia kufanya vibaya kwenye mitihani.

Hali hiyo imewaibua wadau wa elimu na kuiomba Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kutunga sheria ndogo itakayowalazimisha wazazi kutoa chakula kwa ajili ya watoto wao kwa lazima.

Akizungumza kwenye kikao cha wadau wa elimu wilayani Mbarali juzi, Mratibu wa Elimu Kata ya Mapogoro, Francis Makombe, alisema mara kwa mara wamekuwa wakiwahamasisha wazazi pamoja na walezi kuchangia chakula shuleni, lakini wamekuwa wakaidi.

Alisema licha ya wilaya hiyo kuwa wazalishaji wakubwa wa mpunga, lakini mwitikio ni mdogo na kusababisha watoto kufanya vibaya kwenye mitihani yao kutokana na kukosa chakula shuleni.

Alisema kutungwa kwa sheria ndogo kutasaidia kuwabana wazazi na kulazimika kuchangia chakula kwa lazima kwa kuwa wakikaidi watachukuliwa hatua.

"Tumejitahidi sana kuwahamasisha wazazi pamoja na walezi kuchangia chakula shuleni, tumetumia mikutano ya hadhara na mikusanyiko mingine ili kuhamasisha zoezi hili, lakini bado mwitikio ni mdogo, nafikiri tukitunga sheria ndogo za kuwabana itasaidia chakula kipatikane kuliko ilivyo sasa tunabembeleza wakati elimu ni kwa manufaa ya watoto wetu na jamii," alisema Makombe.

Diwani wa Mapogoro, Paul Kitta, alisema atapeleka hoja ya dharura kwenye vikao vya baraza la madiwani kutoa tamko wazazi kuchangia chakula shuleni pamoja na kutungwa kwa sheria ndogo.

Alisema kuna umuhimu mkubwa kuwapo chakula shuleni kwa kuwa itasaidia watoto kusoma kwa utulivu kwa sababu hawatakuwa na njaa na wataelewa masomo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Misana Kwangura, alisema kupatikana kwa chakula shuleni kutakuwa ni mwarobaini wa kuongeza ufaulu kwa watoto na kuifanya wilayani hiyo kushika nafasi za juu kitaaluma.

# Maharagwe soya yapata soko nchini China

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

SERIKALI imesema imejipanga kuongeza uzalishaji wa zao la maharagwe aina ya soya ili kuchangamkia soko lake linalopatikana nchini China yenye uhitaji wa zaidi ya tani milioni moja kwa mwaka.

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, alitoa kauli hiyo jana baada ya kutembelea na kukagua eneo la Nkung'ungu lenye ukubwa wa ekari 17, kati ya ekari 100,000 ambalo Mkoa wa Mbeya umelitoa wilayani Chunya kwa ajili ya kilimo cha maharagwe ya soya.

Alisema wanafanya hivyo ikiwa ni jitihada za serikali kuhakikisha wakulima wananufaika na kilimo chao na tayari soko la uhakika lipo, kinachosubiriwa ni kuzalisha kwa wingi mazao hayo ili kukidhi mahitaji nchini China.

Alisema mwaka jana Tanzania ilifanikiwa kuiuzia China maharagwe ya soya tani 50,000 kati ya 1,000,000 zinazohitajika nchini humo kwa mwaka.

Alisema katika kukidhi mahitaji ya soko hilo na Tanzania wakiwa ni wabia namba moja, amepatikana mwekezaji wa ekari zote 100,000 zilizotolewa wilayani Chunya kwa ajili ya kuanza kilimo hicho.

"Tumempata mwekezaji ambaye kwa masharti yetu amekubali, kwanza kutupatia mbegu bora na teknolojia za kisasa, ambazo wakulima wetu watazitumia katika kuzalisha zao hilo, tunatamani sasa mkulima azalishe kwa tija na kunufaika na shughuli yake kuliko ilivyokuwa hapo awali ambapo anatumia nguvu kubwa kulima, lakini mavuno kidogo," alisema Mavunde.

Alisema kwa Tanzania serikali imefanya utafiti kwa maeneo mbalimbali ya mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na kujiridhisha yanafaa kwa kilimo cha maharagwe ya soya na kutoa wito kwa wakulima kujiingiza kwenye kilimo hicho ambacho tayari kina soko la uhakika.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Chunya, Mbunge wa Jimbo la Lupa, Masache Kasaka, alisema wamejipanga kuzalisha kwa wingi zao hilo.

Aliwaomba wataalamu wa kilimo kutoa elimu ya kutosha ili kuwasaidia kuzalisha kwa wingi na kupata faida nyingi ikiwamo fedha na kuongeza thamani ya zao hilo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema kilimo cha soya kimekuja kama mbadala wa tumbaku na mkulima akipata mavuno kidogo kwenye zao moja atanufaika na jingine.

Alisema kwa sasa mkulima atakuwa na chaguo la kulima zao analotaka kulingana na majira kuliko ilivyokuwa awali hususani kwa wakulima Wilaya ya Chunya ambao baadhi yao wanategemea zaidi kilimo cha tumbaku.



## Watakiwa kufuata mwongozo uhifadhi maeneo ya bahari

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANANCHI wametakiwa kufuata mwongozo uliotolewa na Idara ya Uhifadhi kwa taratibu za kisheria zilizowekwa na serikali ili kuepusha athari mbalimbali zinazojitokeza katika maeneo ya hifadhi za bahari pamoja na upotevu wa vivutio vya utalii.

Hayo yalielezwa na Meneja wa Hifadhi ya Tumbatu (TUMCA), Said Shaib Said, kutoka Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi katika kikao na manahodha wa boti za kupeleka watalii katika maeneo ya hifadhi za bahari Nungwi, Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa lengo la kutunza mazingira ya bahari ili kuufanya utalii kuwa endelevu.

Said alisema kuna baadhi ya wageni wana tabia ya kuwalisha vyakula holela viumbe vya baharini ikiwamo kasa na kuwabeba kwa ajili ya kupiga nao picha jambo ambalo ni kosa kisheria na kupelekea athari kubwa kuliko faida inayopatikana.

Alisema umefikia wakati kwa jamii kubadilika hususani wenye shughuli za kitalii kuacha tabia ya kutupa taka za plastiki katika hifadhi za bahari ili kukuza sekta ya uchumi wa buluu kuweka mazingira safi na salama kwa ajili ya afya ya baharini na ufukweni.

Naye Ofisa Mipango, Mchanga Said Khamis, kutoka Idara ya Uhifadhi wa maeneo ya bahari Zanzibar, alisema ushirikiano wa pamoja unahitajika kwa manahodha wa vyombo vya utalii kuepuka kutupa nanga katika matumbawe ili kuziacha rasilimali za bahari kuwa salama.

Mshauri wa uchumi wa buluu, Kris Horill, aliwataka manahodha wanaopeleka wageni katika maeneo ya hifadhi kuwa mstari wa mbele katika suala la ulinzi shirikishi wa rasilimali za bahari kutunza mazingira ya bahari ili kuleta mabadiliko katika sekta ya uchumi wa buluu kupitia utalii.

Kwa upande wao washiriki wa kikao hicho wameziomba taasisi husika kuzidi kuwapatia elimu ya muongozo uliotolewa na idara ya uhifadhi kutokana na umuhimu wa kutunza viumbe wa baharini kwa ajili ya kutanua sekta ya utalii nchini na maendeleo kwa taifa.



Muhammed Said Tausiri mpishi na muuzaji wa halua akiwa katika eneo lake la biashara Mji wa Chakechake Pemba, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wawakilishi waunga mkono visiwa 10 kukodishwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wameunga mkono hatua ya Serikali ya Zanzibar kukodisha visiwa 10 kwa wawekezaji kwa ajili ya kuingiza mapato.

Wakichangia bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2022-2023 katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, walisema ni uamuzi sahihi katika kuinufaisha nchi kupata fedha za kigeni.

Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni, Sulubu Kidongo Amour, alisema kwa muda mrefu visiwa vidogo vipo, lakini hakuna aliyevishughulikia na kubuni wazo la kuvikodisha kwa uwekezaji.

Kidogo alimpongeza Rais Hussein Ali Mwinyi kwa uamuzi wake wa kuvikodisha visiwa kwa wawekezaji hatua ambayo itaongeza mapato mengi kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Naye mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini, Machano Othman Said, aliunga mkono uamuzi huo wa kuwekeza katika visiwa vidogo ambavyo vitaongeza mapato ya nchi.

Alikiri kwa muda mrefu visiwa hivyo havikuwa na uwekezaji wenye tija uliofanywa na kwa kiasi kikubwa umelikosesha taifa mapato.

"Mheshimiwa Naibu Spika naunga mkono uamuzi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuwekeza katika visiwa vidogo kwa ajili ya kuingiza kipato kikubwa kuliko kuviachia visiwa vikiwa havina uwekezaji," alisema. Kwa upande wake, Mwakilishi wa Jimbo la Mtoni, Hussein Ibrahim Makungu, alimpongeza Rais Mwinyi kwa uamuzi wake wa kuvikodisha visiwa hivyo 10 kwa wawekezaji ambavyo tayari vimeingiza fedha nyingi katika miradi ya maendeleo.

Alizitaja baadhi ya nchi duniani zilizopiga hatua katika utalii wake kwa kuchukua uamuzi wa kukodisha visiwa kwa wawekezaji nje ya nchi.

Aliitaja nchi ya Indonesia ambayo imepiga hatua kubwa katika utalii wake baada ya kuchukua uamuzi wa kukodisha visiwa vyake vingi kwa wawekezaji na kuendeleza utalii na kuingiza pato kubwa la uchumi.

"Mheshimiwa Naibu Spika naunga mkono kwa asilimia mia moja uamuzi wa serikali wa kukodisha visiwa vidogo kwa wawekezaji hatua ambayo itaongeza mapato yetu," alisema Makungu.

# Serikali yashauriwa kutafuta madaktari

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAKATI Serikali ya Zanzibar ikiendelea na ujenzi wa hospitali katika kila wilaya Unguja na Pemba, Wizara ya Afya imetakiwa kutayarisha wafanyakazi watakaotoa huduma katika hospitali hizo ili kuepuka tatizo la uhaba wa wataalamu ikiwamo madaktari.

Hayo yalielezwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi, Miraji Khamis Mussa, wakati akiwasilisha maoni ya kamati hiyo kwa mwaka wa fedha 2022-2023 katika Baraza la Wawakilishi, Chukwani Unguja.

Alisema serikali inajenga hospitali hiyo kupitia fedha za ahueni za kupambana na ugonjwa wa UVIKO-19 kwa ajili ya kuleta maendeleo katika sekta muhimu za uchumi.

Alisema Serikali ya Zanzibar imepata mgao wa Sh. bilioni 230 kwa Serikali ya Tanzania kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ambazo kwa upande wa Zanzibar zimelenga utekelezaji wa miradi ya huduma za jamii ikiwamo ujenzi wa shule, hospitali na kuwawezesha wajasiriamali kiuchumi.

Alizitaka wizara ambazo zinatekeleza miradi ya fedha hizo za ahueni kuhakikisha fedha hizo zinatumika vizuri na kuifuatilia kwa karibu miradi yote inayotekelezwa katika taasisi husika kwa ajili ya kukidhi malengo na matarajio yake.

Alisema ujenzi wa hospitali 10 za wilaya ni muhimu ambao utalipatia ufumbuzi tatizo la wananchi kutembea masafa marefu kufuata huduma za afya ikiwamo wajawazito na watoto.

"Mheshimiwa Naibu Spika kamati ya bajeti inaunga mkono moja kwa moja matumizi ya Sh. bilioni 36 kwa ajili ya sekta ya afya ikiwamo ujenzi wa hospitali 10 za wilaya pamoja na moja ya mkoa, jibu la tatizo la huduma za afya limepatiwa ufumbuzi wake wa kudumu," alisema.

Alipongeza serikali kutenga Sh. bilioni 36 kwa ajili ya kuwawezesha wajasiriamali wa uvuvi wa bahari kuu na kuwawezesha kuvuna rasilimali za baharini kikamilifu ili kujikwamua kiuchumi.

Aidha, alisema hadi sasa pato katika sekta ya uvuvi na mazao ya baharini ni asilimia 10 wakati sekta hiyo imeajiri watu wengi waliozungukwa na bahari ya visiwa vya Unguja na Pemba.

Alipongeza ujenzi wa boti za uvuvi zipatazo 577 ambazo zitawawezesha wavuvi maeneo ya mwambao wa bahari kuvua katika bahari kuu yenye kiwango kikubwa cha samaki ambacho hakijavunwa hadi sasa.

# Rais Macron akataa Waziri Mkuu kujiuzulu

**PARIS,** Ufaransa

WAZIRI Mkuu wa Ufaransa Elisabeth Borne, amewasilisha barua yake ya kujiuzulu kwa Rais Emmanuel Macron, ambaye amepinga uamuzi wake huo.

Ikulu ya nchi hiyo ilieleza kwamba Borne amechukua hatua ya kujiuzulu ili serikali iweze kuendelea na majukumu yake na kuchukua hatua katika siku zijazo.

Hata hivyo, Rais Macron amefanya mashauriano muhimu ya kisiasa ili kubaini suluhisho linaloewezekana katika kuwahudumia Wafaransa.

Hata hivyo, Waziri Mkuu alikutana kwa mazungumzo na serikali nzima mapema alasiri ya jana katika ofisi yake Matignon.

Viongozi sita wa kisiasa wataanza kukutana na Macron kutafuta suluhu zinazoweza kujenga.

Viongozi ambao alikutana nao jana ni Christian Jacob kutoka chama cha Les Républicains, Olivier Faure (Chama cha Kisoshalisti), François Bayrou (chama cha Kidemokrasia), Stanislas Guerini (chama cha Renaissance), Marine Le Pen (chama cha RN) na Fabien Roussel (Chama cha Kikomunisti).

Mashauriano hayo yataendelea leo ambapo rais Maron atawapokea viongozi wengine kutoka chama cha kijani (Les Verts), Julien Bayou, kiongozi nambari mbili wa chama cha La France insoumise (LFI), Adrien Quatennens, na kiongozi wa kundi la LFI katika Bunge la Kitaifa, Mathilde Panot.

Adrien Quatennens na maofisa wengine kadhaa wa LFI walitaka kujiuzulu kwa Waziri Mkuu Élisabeth Borne, ambaye hatakuwepo kwenye mikutano na vyama vya kisiasa. **RFI**

# Ukraine yalalama Russia kuongeza mashambulizi

**KYIV,** Ukraine

SERIKALI ya Ukraine imesema Russia inazidi kushambulia mji wa viwanda wa Lysychansk katika eneo la Donbas mashariki mwa nchi hiyo.

Mji huo umekuwa kitovu cha mapigano makali kwa wiki kadhaa sasa kati ya jeshi la Ukraine na vikosi vya Russia. Gavana wa Lugansk, Sergiy Gaiday, alisema katika taarifa yake kwamba mapigano katika ukanda wa viwanda wa Severodonetsk yamechacha na kuna uharibifu mkubwa wa majengo.

Gaiday alisema mtu mmoja amethibitishwa kuuwawa katika mashambulizi makali ya makombora yaliyoendelea jana kutwa nzima na kuharibu kabisa makazi ya watu na kituo kimoja cha polisi.

Gavana huyo pia alieleza mapigano yanaendelea katika kiwanda cha kemikali cha Azot mjini Severodonetsk ambako mamia ya raia wanaaminiwa wamejificha.

**Mkuu mpya aliyeteuliwa wa Jeshi la Uingereza alisema nchi yake na washirika walihitaji kuwa na uwezo wa kushinda vita vya ardhini na Russia.**

Wakati haya yakiarifiwa Rais wa nchi hiyo, Volodymir Zelensky, ameuambia Umoja wa Afrika hapo jana kwamba bara la Afrika limetekwa mateka na uvamizi wa Russia nchini Ukraine ambao umesababisha uhaba wa chakula na kuzua hofu ya kutokea mgogoro wa chakula barani humo.


Nchi za Magharibi lazima zijiandae kuendelea kuunga mkono Ukraine katika vita vinavyoweza kudumu kwa miaka mingi, mkuu wa Nato ameonya.

Katibu Mkuu Jens Stoltenberg alisema gharama za vita ni kubwa, lakini bei ya kuiruhusu Russia kufikia malengo yake ya kijeshi ni kubwa zaidi.

Waziri Mkuu wa Uingereza Boris Johnson pia ameonya kuhusu mzozo wa muda mrefu.

Mkuu mpya aliyeteuliwa wa Jeshi la Uingereza alisema nchi yake na washirika walihitaji kuwa na uwezo wa kushinda vita vya ardhini na Russia.

Jenerali Sir Patrick Sanders, ambaye alianza kazi hiyo wiki jana, alisema katika ujumbe wake wa ndani ulioonekana na BBC, alisema "Uvamizi wa Russia nchini Ukraine unasisitiza lengo letu kuu kulinda Uingereza na kuwa tayari kupigana na kushinda vita vya ardhini." **BBC**



Rais wa Kenya Uhuru Kenyatta, akimkaribisha Rais wa Rwanda, Paul Kagame katika Ikulu ya Nairobi kwa ajili ya mazungumzo ya wakuu wa nchi za Afrika Mashariki juzi. **PICHA: BBC**

# Viongozi EAC wakubaliana kupeleka jeshi DRC

**NAIROBI,** Kenya

VIONGOZI wakuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) wamechukua hatua nyingine kuelekea kuunda kikosi cha kijeshi cha kikanda kitakachosaidia kuleta amani mashariki mwa DRC.

Waliafikiana uamuzi huu katika mkutano wao uliofanyika Jumatatu jijini Nairobi, nchini Kenya.

Wakuu wa nchi 6 kati ya 7 za EAC walihudhuria ikiwamo Kenya, DRC, Rwanda, Burundi, Uganda na Sudan Kusini. Tanzania iliwakilishwa na balozi wake.

Mkutano huo ulidumu saa nne, viongozi hao walikubaliana kupelekwa kwa wanajeshi wa kikanda kukabiliana na waasi wa M23.

Kulingana na ofisi ya rais wa DRC, kikosi hicho kitawekwa chini ya amri ya kijeshi ya Kenya. Kitaanza kufanya kazi katika wiki zijazo na jeshi la Rwanda halitashiriki katika kikosi hicho.

DRC ilisema siku ya Jumanne kwamba haitaki Rwanda katika kikosi hicho, kwa vile inaituhumu kuwaunga mkono waasi wa M23, jambo ambalo Rwanda inakanusha.

Taarifa ya pamoja iliyotolewa na ofisi ya rais wa Kenya, inabaini kwamba wakuu wa nchi hizo wamepitisha msururu wa nyaraka ambazo zinafafanua hasa mamlaka na muundo wa vikosi cha kikanda, kazi yake na jinsi wanajeshi kutoka mataifa yaliyotajwa watashiriki katika kikosi hicho watakavyotawanywa katika maeneo mbalimbali mashariki mwa DRC.

Katika taarifa hiyo wakuu wa nchi za EAC wametoa wito wa kusitishwa mara moja kwa mapigano na waasi kuondoka katika maeneo waliyodhibiti hivi karibuni, wakimaanisha, mji wa kimkakati wa Bunagana ulio chini ya udhibiti wa waasi wa M23 tangu wiki moja iliyopita. **RFI**

# Bennett kulivunja Bunge na kuitisha uchaguzi

**TEL AVIV,** Israel

SERIKALI ya mseto ya Israel inayoondoka madarakani itaharakisha muswada wa sheria wiki hii kulivunja bunge la nchi hiyo ili kuruhusu uchaguzi wa mapema kufanyika.

Hatua hiyo ilifikiwa baada ya hapo jana Waziri Mkuu wa Israel Naftali Bennett kutangaza angelivunja muungano wa vyama vinane, mwaka mmoja tangu aliposhika madaraka.

Katika mkutano na waandishi wa habari Bennett, alisema haukuwa uamuzi rahisi kuivunja serikali lakini ameuita kuwa ni uamuzi sahihi kwa Israel.

Ameahidi makabidhiano ya amani ya madaraka na kuorodhesha mafanikio ya serikali yake.

Wimbi la wabunge kukihama chama chake cha Yemina imeufanya muungano wake kupoteza wingi wa viti bungeni. Bennett amekubali kwamba waziri wa mambo ya nje Yair Lapid atachukua hatamu kama waziri mkuu kwa sasa. Kura inatarajiwa kupigwa bungeni wiki ijayo. **DW**

HABARI MICHEZO

# SIMBA YATUA UHAMIAJI VIBALI VYA KOCHA, WAWA 'BAIBAI'

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Simba imesema tayari imeshamalizana na kocha mpya atakayekuja kuinoa timu hiyo kuanzia msimu ujao wa mashindano, wanachofanya sasa ni taratibu za uhamiaji ili aweze kutua nchini wakati wowote kuanzia sasa.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu ya hiyo, Ahmed Ally, alisema taratibu zote za mwisho zimekamilika za kocha huyo kuja nchini na kutazama mechi mbili za mwisho, lakini akaongeza kuwa hawatoweka hadharani jina la kocha huyo kwa sababu za kiusalama na kibiashara.**

"Taratibu za mwisho kabisa kocha kuja kuanza kazi zimekamilika, lakini zipo taratibu za uhamiaji ambazo viongozi wanazikamilisha, tunategemea akitua aitazame timu yetu kwenye mechi mbili dhidi ya Prisons na Mbeya Kwanza tukiwa nje ya Dar es Salaam.

Hatuwezi kumtaja kwa sasa kwa sababu dunia ya sasa ni ya kiushindani, leo unaweza kumtangaza, kesho ukasikia kuna watu wamempandia dau wamempeleka sehemu nyingine, unajua hivi sasa Simba inatumika kama jicho la watu, ukimtaja tu mchezaji au kocha watu wote wanavamia huko, ndiyo maana tumeamua kuwa na usiri mkubwa," alisema Ahmed.

Sababu nyingine ameitaja kuwa ni ya kibiashara, kwani pamoja na kuwafanyia 'sapraizi' wanachama na mashabiki wa Simba, lakini pia kuingiza mapato kwenye mitandao ya kijamii ya klabu yao pale watakapokuwa wakimtangaza.

"Lakini tunafanya 'sapraizi' ili tukija kutangaza wanachama na mashabiki wetu wafurahi, kama vile haitoshi tuje tuiuze hiyo habari ili klabu ijipatie mapato," alisema.

Hata hivyo, zipo tetesi kuwa kocha wa timu hiyo huenda akawa ni Jozef Vukusic raia wa Slovakia.

Wakati huo huo, klabu hiyo imetangaza kumalizana na mchezaji Pascal Wawa aliyedumu kwenye klabu hiyo kwa misimu minne. Kwenye mtandao wa instagram wa klabu hiyo, iliandika kuwa mchezaji huyo hatokuwa sehemu ya kikosi cha timu hiyo msimu ujao.

"Ahsante Paschal Wawa. Baada ya kutumikia timu yetu kwa misimu minne, Pascal Wawa hatakuwa sehemu ya kikosi chetu cha msimu ujao.

"Mkataba wake utamalizika mwisho wa mwezi huu na mchezo wa Alhamisi dhidi ya Mtibwa Sugar utakuwa wake wa mwisho," uliandika mtandao wa klabu hiyo.



Spika wa Bunge la Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson (mrefu aliyevaa miwani) na Salma Kikwete (aliyevaa fulana ya mikono mirefu ndani), ambaye ni mke wa Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Mrisho Kikwete, wakiwa na baadhi ya wachezaji wa Bunge Queens katika picha ya pamoja na wachezaji wa Taswa Queens. Timu ya Bunge Queens iliifunga Taswa Queens mabao 15-13 katika mchezo wa kirafiki uliochezwa Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# *Spika Tulia azimwagia sifa Bunge SC, Taswa SC*

Na Mwandishi Wetu

SPIKA wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson, amezipongeza timu ya Waandishi wa Habari za Michezo nchini (Taswa SC) na Bunge SC kwa 'kupromoti' michezo baada ya kuonyesha mfano kwa vitendo kwa kucheza katika mechi mbalimbali.

Spika Tulia alisema hayo wakati wa mechi maalum ya kirafiki kati ya Taswa SC na Bunge SC iliyofanyika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma na Taswa SC kuibuka na ushindi wa mabao 2-0.

Alisema amevutiwa na jinsi wabunge na waandishi wa habari wakionyesha vipaji vyao katika mpira wa miguu na netiboli, jambo ambalo litawafanya vijana kuiga mfano wao na kupata wachezaji nyota wa timu za taifa.

"Kwa kweli hii imenivutia sana kwani tutawafanya vijana kuiga mfano na kuwa na wachezaji bora, nawatakia kila la kheri katika jambo hili," alisema Tulia ambaye alikuwa miongoni mwa wachezaji walioichezea timu ya Netiboli ya Bunge Queens iliyoifunga Taswa Queens mabao 15-13.

Mbali ya Ackson, pia Mama Salma Kikwete ni mmoja wa wachezaji nyota wa timu ya Bunge Queens ambayo inajiandaa na michuano ya Bunge la Afrika Mashariki iliyopangwa kufanyika Juba, Sudan Kusini.

Kwa upande wa Meneja Masoko wa Kampuni ya Michezo ya Kubahatisha ya M-Bet Tanzania, Allen Mushi, alisema kuwa amefurahishwa na timu zote mbili na kampuni yao ipo tayari kuzisaidia timu zote katika shughuli mbalimbali za michezo na kijamii.

"M-Bet Tanzania inajisikia faraja zaidi kushirikiana na Taswa SC katika kufanikisha ziara na tukio hili, pia tupo tayari kusaidia timu ya Bunge SC katika masuala mbalimbali," alisema Mushi.

Naye Mwenyekiti wa Taswa SC, Majuto Omary, aliipongeza timu ya Bunge SC na Kampuni ya M-Bet Tanzania kwa kufanikisha lengo lao la kucheza na waheshimiwa wabunge kwa mara ya pili.

Nahodha wa timu ya Bunge SC, Cosato Chumi, alisema wamepata kipimo kizuri kuelekea michuano ya Afrika Mashariki na kuipongeza Taswa SC kwa mchezo mzuri.

Ushindi huo wa Taswa SC wa mabao 2-0 dhidi ya Bunge SC, unaifanya kuendeleza rekodi yake ya kutofungwa mwaka huu. Mabao ya Taswa SC yalifungwa na Waziri Idd na Zicco George.

Katika netiboli, Bunge Queens iliendelea 'kuinyanyasa' Taswa Queens baada ya kuichapa kwa mabao 15-13.

# Daudi aibuka kinara wa Lugalo Open

Na Saada Akida

MCHEZAJI wa gofu wa Klabu ya Lugalo, Isihaka Daudi, amefanya vizuri kwa kuibuka mshindi katika shindano la TFS Lugalo Open 2022 lililomalizika juzi jijini Dar es Salaam.

Daudi aliibuka kinara kwa kupiga mikwaju 75 siku ya kwanza na 70 siku ya pili, hivyo kupata jumla 145, huku nafasi ya pili ikienda kwa Victor Joseph kutoka Klabu ya Dar Gymkhana kwa mikwaju 75 siku ya kwanza na 75 siku ya pili ikikamilisha jumla 150.

Upande wa makundi Divisheni A, mshindi wa kwanza ni Nicholous Chitanda mikwaju ya jumla 144 akifuatiwa na John Hiza akipiga jumla ya mikwaju 145, wachezaji wote wakitoka Lugalo.

Katika kundi la Divisheni B, mshindi wa kwanza ni Marcell Lubuva wa Lugalo aliyefungana na Michael Palangyo wa klabu ya Kili gofu Arusha wote wakipata jumla ya mikwaju 142.

Divisheni C, mshindi ni Cyril Brown kutoka Klabu ya Kili Gofu, akipiga jumla ya mikwaju ya143 na akifuatiwa na Nsajigwa Mwansasu wa Lugalo aliyechapa jumla ya mikwaju 145.



Kwa upande wa wanawake mshindi ni Angel Eaton kwa mikwaju 82 siku ya kwanza na 77 siku ya pili ikikamilisha jumla 159, mshindi wa pili ni Victoria Elias wa Lugalo mikwaju 82 siku ya kwanza na 80 siku ya pili, hivyo kutimiza mikwaju 162 kwa jumla ya siku hizo wote wakitoka Klabu ya Lugalo.

Kwa wacheza waliopiga umbali mrefu mshindi wa upande wa wanaume ni Isihaka Daudi, akishinda kwa mara nyingine na wanawake ni Ayne Magombe wote kutoka Klabu ya Lugalo.

Katika upigaji wa mpira wa karibu kabisa na shimo kwa mwanaume mshindi ni Elisha Fadhil kwa wanawake ni Angel Eaton, kwa wachezaji wazee kwa wanaume mshindi wa kwanza ni Joseph Tairo mikwaju jumla 152 akifuatiwa na Julius Mbilinyi 157.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**RAPHINHA ANUKIA ARSENAL**

ARSENAL wanakaribia kumsajili mshambuliaji wa Brazil, Raphinha, 25, kutoka Leeds United, huku nia ya Barcelona kumnunua mchezaji huyo ikiwa imepungua. ***(Goal)***

**RICHARLISON AWANIWA**

CHELSEA wameungana na Tottenham Hotspur kutaka kumsajili mshambuliaji wa Brazil, Richarlison, 25, kutoka Everton, ambao wanataka zaidi ya pauni milioni 50 kwa mchezaji huyo. ***(Mail)***

**GRANOVSKAIA KUONDOKA**

MARINA Granovskaia, ambaye alichukua jukumu la uhamisho wa wachezaji katika klabu ya Chelsea chini ya mmiliki wa zamani, Roman Abramovich, anakaribia kuondoka katika klabu hiyo. ***(Guardian)***

**BROJA HUYOOO WEST HAM**

KLABU ya West Ham inatazamiwa kutoa takriban pauni milioni 30 kwa mshambuliaji wa Chelsea na Albania, Armando Broja, 20, ambaye alicheza kwa mkopo Southampton msimu uliopita. ***(Sky Sports)***

**ERIKSEN ATAKIWA SPURS**

KLABU ya Tottenham Hotspur iliwasiliana na kambi ya mchezaji wa Denmark, Christian Eriksen, 30, wiki chache zilizopita, lakini hawajaonyesha tena nia ya kumtaka mchezaji wao huyo ambaye alitumia kipindi cha pili msimu uliopita Brentford. ***(Football London)***

**TEN HAG NA DE JONG**

KOCHA mpya wa Manchester United, Erik ten Hag ameiambia klabu hiyo kuwa anataka kuwasajili Christian Eriksen na kiungo wa kati wa Barcelona na Uholanzi, Frenkie de Jong, 25. ***(Goal)***

**EVANILSON AWINDWA UNITED**

KLABU ya Manchester United imekuwa na ofa ya pauni milioni 55 kwa mshambuliaji wa Brazil, Evanilson, 22, iliyokataliwa na Porto, lakini miamba hiyo ya Old Trafford inapanga kutoa ofa mpya kwa mchezaji huyo. ***(O Jogo, via Mail)***

**MARTINEZ LULU ENGLAND**

BAADA ya kushindwa kumsajili mlinzi, Jurrien Timber, 21, Manchester United inaweza kuchukua hatua ya kumsajili mchezaji mwenzake wa Ajax, Lisandro Martinez. Beki huyo wa kati wa Argentina mwenye umri wa miaka 24, pia analengwa na Arsenal. ***(Mirror)***

**VILLA KUMUUZA MCGINN**

KLABU ya Aston Villa ipo tayari kusikiliza ofa kwa kiungo wa kati wa Scotland, John McGinn, 27, msimu huu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

**TREZEGUET KUTIMKIA UTURUKI**

WINGA wa Misri, Trezeguet, 27, anakaribia kuondoka Aston Villa na kujiunga na Trabzonspor ya Uturuki kwa takriban pauni milioni 3. ***(Mail)***

**COOPER KUSAINI MKATABA**

KOCHA wa Nottingham Forest, Steve Cooper, ambaye alikiongoza kikosi chake kupanda Ligi Kuu msimu uliopita, yuko mbioni kusaini mkataba mpya wa muda mrefu na klabu hiyo. ***(Nottinghamshire Live)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# GUARDIOLA: NINAIMANI SILVA ATABAKI MAN CITY

**Nadhani atakaa nasi, hiyo ni hisia yangu kama ilivyo leo, hatujui nini kitatokea kwenye...**

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola anaimani kuwa Bernardo Silva atasalia katika klabu hiyo, ingawa aliapa kutokaa na mchezaji yeyote asiye na furaha.

**Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno, Silva amekuwa akihusishwa na kuhamia Barcelona baada ya kukaa kwa miaka mitano hapo kwenye Uwanja wa Etihad, huku Xavi akitaka kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27.**

Ilisemekana kwamba, Silva aliweka wazi hisia zake za kutaka kuondoka City mwaka jana, lakini mchezaji huyo wa zamani wa Monaco alibaki na kuwa nguvu muhimu wakati timu hiyo ya Guardiola iliposhinda taji la Ligi Kuu kwa mara ya nne ndani ya misimu mitano.

Hata hivyo, Guardiola amemwagia maji baridi juu ya uvumi kwamba Silva atahama kabla ya kuanza kwa msimu wa 2022-23 wakati akizungumza kufuatia kutangazwa kwa mechi ya kirafiki ya City dhidi ya klabu yake ya zamani, Barcelona.

"Nadhani Bernardo Silva atakaa nasi, hiyo ni hisia yangu kama ilivyo leo," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari.

"Hatujui nini kitatokea kwenye dirisha la usajili na tumekuwa tukisema kwamba tunataka wachezaji ambao wanataka kuwa kwenye klabu yetu wawe na furaha.

"Lakini tunamthamini sana Bernardo na tunamtegemea kwa msimu ujao."

City wamemleta Erling Haaland tayari dirisha hili la usajili, huku wakiripotiwa kutaka kuwasajili beki wa kushoto wa Brighton and Hove Albion, Marc Cucurella na kiungo wa Leeds United, Kalvin Phillips.

Hata hivyo, Raheem Sterling na Gabriel Jesus wote wanaripotiwa kutaka kuondoka, huku Chelsea na Arsenal zikiwa mstari wa mbele kuwawania.

Mechi kati ya City na Barca itafanyika Agosti 24 katika mchezo wa hisani kutafuta fedha.

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,008,5

MECHI KALI
YOUNG AFRICANS
VERSUS
POLISI TANZANIA
1 | 1.26
X | 5.00
2 | 12.00

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KOCHA MISRI AMSHUTUMU SALAH



**CAIRO,** Misri

MOHAMED Salah hajafaulu "chochote" akiwa na Misri na nyota huyo wa Liverpool lazima ainue kiwango chake wakati akichezea timu ya taifa, kwa mujibu wa kocha wa zamani wa 'Pharaohs' hao, Hassan Shehata.


Hata hivyo, Waziri wa zamani wa Michezo na Vijana wa Misri, Khaled Abdel Aziz, amemtetea mshambuliaji huyo, akimtaja kuwa balozi mzuri na mtu anayeunganisha nchi hiyo.

Salah alifunga mabao 31 na kutoa asisti 15 katika michuano yote kwa Liverpool waliposhinda taji la EFL na Kombe la FA msimu uliopita, pia walimaliza kama washindi wa pili katika Ligi Kuu ya England na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Lakini mshambuliaji huyo alikabiliwa na kampeni ya kufadhaisha zaidi kwenye timu ya taifa, wakati Misri ilipopoteza fainali ya Kombe la Mataifa ya Afrika kwa mikwaju ya penalti dhidi ya Senegal, Februari na kukumbwa na hali kama hiyo katika mchujo muhimu wa kufuzu Kombe la Dunia Machi - huku Salah akikosa nafasi hiyo.

Matokeo hayo ya kukatisha tamaa yamemfanya Shehata, ambaye aliifundisha Misri kutoka mwaka 2004 hadi 2011 na kushinda mataji mfululizo ya Kombe la Mataifa ya Afrika mwaka 2006, 2008, na 2010, kuomba Salah aboreshe kiwango chake.

"Sote tunajua kwamba, Salah ni mmoja wa nyota wa dunia na si mmoja tu wa nyota wa Misri," alisema akiambia Sada al-Balad. "Tuzo alizotwaa na mabao aliyofunga yanampa haki ya kuwa nyota wa juu.



## Rudiger afichua kuikataa Barca

**MADRID,** Hispania

ANTONIO Rudiger amefichua kuwa alifanya uamuzi wake wa kusaini Real Madrid Aprili na akaipuuza ofa ya Barcelona.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani amesaini mkataba wa miaka minne na mabingwa hao wa Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kumalizika kwa mkataba wake na Chelsea, na hivyo kuhitimisha miaka mitano aliyokaa pale Stamford Bridge.

Muda wake akiwa na 'The Blues' hao, ulimfanya kubeba Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2020-21, Kombe la FA msimu wa 2017-18 na Ligi ya Europa msimu wa 2018-19, akicheza zaidi ya mechi 200 katika mashindano yote.

Rudiger alieleza kuwa Madrid walifanya mawasiliano na wakala wake kwa mara ya kwanza Septemba kabla ya kufuatilia zaidi Aprili, alipofanya uamuzi wa kujiunga na kikosi cha Carlo Ancelotti - na kuongeza kuwa alikataa kwenda kwa wapinzani wa 'Los Blancos', Barca.

"Mara ya kwanza nilipozungumza na Ancelotti ilikuwa Aprili na mawasiliano hayo yalikuwa muhimu sana, ndipo nilipoamua kuichezea klabu hii," alisema akiwaambia waandishi wa habari Jumatatu.

534,842/-

## SUPA JACKPOT
## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 25/06/22 | 22:10 | Club Atletico Alvarado vs Belgrano | 3.50 | 2.90 | 2.33 |
| 02. 25/06/22 | 22:30 | Atletico PR vs Bragantino SP | 2.44 | 3.03 | 3.08 |
| 03. 26/06/22 | 00:00 | DC United vs Nashville | 2.43 | 3.40 | 2.85 |
| 04. 26/06/22 | 00:00 | Colon Santa Fe vs Huracan | 2.35 | 3.28 | 3.13 |
| 05. 26/06/22 | 02:30 | Toronto vs Atlanta United | 2.96 | 3.51 | 2.32 |
| 06. 26/06/22 | 05:00 | San Jose Earthquake vs Los Angeles Galaxy | 2.61 | 3.56 | 2.56 |
| 07. 26/06/22 | 05:30 | Portland Timbers vs Colorado Rapids | 2.26 | 3.43 | 3.12 |
| 08. 26/06/22 | 12:00 | Vissel Kobe vs Urawa Red Diamonds | 2.78 | 3.23 | 2.63 |
| 09. 26/06/22 | 12:00 | Nagoya Grampus vs Kashima Antlers | 2.92 | 3.28 | 2.48 |
| 10. 26/06/22 | 12:00 | Yokohama vs Niigata Albirex | 2.59 | 3.24 | 2.74 |
| 11. 26/06/22 | 12:30 | Kyoto Sanga vs Shonan Bellmare | 2.73 | 3.29 | 2.63 |
| 12. 26/06/22 | 13:00 | Omiya Ardija vs Zwiegen Kanazawa | 2.91 | 3.21 | 2.48 |
| 13. 26/06/22 | 19:00 | Ham-Kam vs Sarpsborg | 2.74 | 3.43 | 2.45 |
| 14. 26/06/22 | 19:00 | Sandefjord vs Tromso | 2.78 | 3.42 | 2.42 |
| 15. 26/06/22 | 19:00 | Stromsgodset vs Lillestrom | 2.73 | 3.42 | 2.46 |
| 16. 26/06/22 | 19:00 | San Lorenzo vs Tigre | 2.84 | 3.30 | 2.54 |
| 17. 26/06/22 | 22:00 | Botafogo RJ vs Fluminense | 2.52 | 3.12 | 2.87 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATANO - 22/06/2022

| MUDAVV | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 1199 | KMC vs Mbeya Kwanza FC | 1.94 | 3.04 | 3.92 |
| 16:00 | 1231 | Penang vs Terengganu | 3.40 | 3.35 | 1.97 |
| 16:00 | 1845 | Gremio Novorizontino SP U20 vs Mirassol FC U20 | 2.19 | 3.49 | 2.80 |
| 18:00 | 1616 | VPS Vaasa vs Honka | 3.14 | 3.24 | 2.12 |
| 18:00 | 2047 | Lietava Jonava vs FK Panevezys | 17.67 | 6.68 | 1.12 |
| 18:00 | 3583 | Valmiera Fk/Bjss vs Rigas Futbola Skola | 2.33 | 3.42 | 2.64 |
| 18:00 | 3886 | Inter Turku vs Lahti | 1.52 | 4.03 | 5.11 |
| 18:00 | 4027 | Neftchi Fargona vs Nasaf Qarshi | 4.80 | 3.28 | 1.70 |
| 18:00 | 4519 | Ilves Tampere vs Hifk | 1.40 | 4.31 | 6.47 |
| 18:00 | 4597 | KuPS Kuopio vs AC Oulu | 1.33 | 4.53 | 7.88 |
| 18:00 | 4615 | Seinajoen JK vs Haka | 2.33 | 3.13 | 2.84 |
| 18:30 | 1686 | Kajha vs OTP FC | 2.27 | 3.24 | 2.85 |
| 18:30 | 3588 | KPV Kokkola vs EIF Ekenas | 3.05 | 3.54 | 2.04 |
| 18:30 | 3824 | Kapa vs PPJ | 1.91 | 3.88 | 3.15 |
| 18:30 | 4513 | FC Lapa vs Kiffen | 6.69 | 5.71 | 1.29 |
| 18:30 | 4572 | Israel U19 vs Austria U19 | 3.34 | 3.54 | 1.93 |
| 18:30 | 4976 | Young Africans vs Polisi Tanzania | 1.31 | 4.32 | 9.63 |
| 18:30 | 5421 | Pif Jalkapallo vs FF Jaro | 4.12 | 3.83 | 1.68 |
| 18:30 | 5677 | Japs vs MP Mikkeli | 2.42 | 3.39 | 2.55 |
| 19:00 | 1700 | Musa Pori vs Grankulla Ifk | 2.22 | 3.67 | 2.65 |
| 19:00 | 2567 | Futbolo Akademija Siauliai vs Zalgiris Kaunas | 3.55 | 3.20 | 2.06 |
| 19:00 | 3099 | IA Sud America vs CA Progreso | 3.14 | 2.89 | 2.29 |
| 19:00 | 4041 | IFK Mariehamn vs HJK Helsinki | 5.87 | 4.11 | 1.46 |
| 19:00 | 4646 | Difaa El Jadidi vs FUS Rabat | 2.75 | 2.90 | 2.55 |
| 19:00 | 5095 | US Ben Guerdane vs US Monastir | 6.00 | 3.30 | 1.64 |
| 19:00 | 5097 | Randesund IL vs Vindbjart | 5.20 | 4.80 | 1.47 |
| 19:00 | 5361 | Salpa Salo vs FC Jazz | 1.86 | 3.87 | 3.28 |
| 19:30 | 1535 | Torslanda IK vs Vastra Frolunda IF | 2.55 | 3.55 | 2.49 |
| 20:00 | 1548 | National Bank vs Zamalek | 4.63 | 3.22 | 1.82 |
| 20:00 | 1920 | IF Algarna vs Umea FC Akademi | 2.16 | 3.86 | 2.64 |
| 20:00 | 2127 | Zalgiris vs Dziugas | 1.08 | 8.02 | 21.53 |
| 20:00 | 2676 | Torns IF vs IFK Malmo | 1.92 | 3.78 | 3.19 |
| 20:00 | 4086 | Nykoping Bis-Trosa vs Vagnharad SK | 1.16 | 6.66 | 11.76 |
| 20:00 | 4633 | FC Volna Pinsk vs Dinamo Minsk | 11.80 | 5.51 | 1.20 |
| 20:00 | 4763 | FC Riga vs FK Auda | 1.32 | 4.70 | 7.64 |
| 20:00 | 5162 | Orebro Syrianska vs FC Stockholm Internazionale | 2.71 | 3.40 | 2.29 |
| 20:00 | 5232 | Landvetter IS vs Savedalens IF | 2.50 | 4.02 | 2.22 |
| 20:00 | 5463 | Eastern Company SC vs Pyramids | 7.80 | 4.60 | 1.37 |
| 20:30 | 2282 | Sandviks IK vs Sund IF | 1.84 | 3.78 | 3.44 |
| 20:30 | 2463 | Lunds BK vs Qviding Fif | 1.92 | 3.55 | 3.60 |
| 20:30 | 2929 | Smedby Ais vs Varmbols FC | 1.25 | 5.90 | 7.67 |
| 20:30 | 3460 | Lidkopings FK vs Stenungsunds IF | 1.82 | 3.93 | 3.39 |
| 20:30 | 3742 | Azam vs Tanzania Prisons | 1.76 | 3.15 | 5.20 |
| 20:30 | 4317 | Vanersborgs IF vs Tvaakers IF | 3.14 | 3.63 | 1.97 |
| 20:30 | 5694 | FC Jarfalla vs IFK Stocksund | 4.83 | 4.73 | 1.47 |
| 21:00 | 1005 | England U19 vs Serbia U19 | 1.51 | 4.14 | 5.12 |
| 21:00 | 1888 | CD Villa Espanola vs Juventud LP | 2.76 | 2.95 | 2.51 |
| 21:00 | 4062 | Miramar Missiones vs Racing Club (URU) | 4.03 | 3.14 | 1.88 |
| 22:15 | 1307 | KV Vesturbaer vs Throttur Vogum | 2.07 | 3.65 | 3.10 |
| 22:30 | 4777 | Al Ahly Cairo vs Ghazl EL Mahallah | 1.33 | 4.63 | 9.46 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# ALIYEDAIWA KUSAJILIWA SIMBA ATANGAZWA SINGIDA BIG STARS

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Mbeya Kwanza, Habib Kyombo, ambaye hadi jana alihusishwa kujiunga na Simba, ameibukia Singida Big Stars baada ya klabu hiyo jana kutangaza rasmi kuingia mkataba wa miaka miwili na mchezaji huyo.

**Jana mchana mtandao wa Instagram wa klabu hiyo uliweka picha ya mchezaji huyo akisaini mkataba mbele ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Muhibu Kanu.**

"Karibu fundi wa mpira uitumikie klabu yako pendwa kwenye msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2022/23.

Kwa muda wa wiki moja sasa, straika huyo wa zamani wa timu za Mbao FC na Singida United, alikuwa akihusishwa kujiunga na Klabu ya Simba huku baadhi ya mashabiki wa soka wakipishana mitazamo juu ya usajili huo. Kabla ya kutangazwa na Singida Big Stars, Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, alishangaa juu ya uwapo wa habari za timu yake kumsajili mchezaji huyo.

"Hizo habari hata mimi nazisikia kwenye mitandao na baadhi ya vyombo vya habari, lakini sisi hatujui chochote, unajua hadi nimekutana na wakala wake na kumuuliza hizi habari za kusajiliwa kwa mchezaji huyo Simba zimetokea wapi, lakini hata yeye akawa hana jibu," alisema Ahmed.

Alisema kuna wakati baadhi ya wachezaji wanaitumia klabu hiyo ili kujipandisha thamani.

Kwa sasa klabu zimekuwa kwenye harakati za usajili, huku wachezaji mbalimbali wa ndani na nje wakihusishwa kwenye klabu za Ligi Kuu Tanzania Bara kwa ajili ya msimu ujao.




Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze (kulia), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu mchezo wao dhidi ya Polisi Tanzania utakaopigwa leo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, pembeni ni Ofisa Habari na Mawasiliano Bodi ya Ligi Kuu Tanzania, Karim Boimanda. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Dulla Boys, Kundemba FC zapanda Ligi Kuu Zanzibar*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Dulla Boys imeungana na Kundemba FC, kupanda Daraja kucheza Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao wa 2022/2023.

Dulla Boys imepanda daraja baada ya kushinda mchezo wake wa mwisho wa Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja kwa jumla ya mabao 3-0 dhidi ya New King.

Kwa matokeo hayo yanaifanya Dulla Boys kupanda daraja huku ikiwaacha wapinzani wao wakuu, Chuoni FC, ambayo licha ya juzi kuibuka na ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Mwembe Makumbi City, lakini ushindi wao haukuisaidia kutokana na tofauti ya alama katika msimamo wa ligi hiyo.

Kwa mujibu wa Kanuni ya mashindano ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), jumla ya timu nne zitapanda daraja kucheza Ligi Kuu kutoka katika Kanda mbili ambazo ni Unguja na Pemba.

Kwa upande wa Pemba timu zilizopanda daraja ni Chipukizi FC na timu Kongwe katika Soka la Zanzibar, Jamhuri SC.

Aidha, kwa upande wa timu zilizoshuka daraja ni New Power FC, ambayo ilishindwa kujilinda baada ya kutoka suluhu dhidi ya Gulioni FC.

Katika mchezo huo, Gulioni FC ilikuwa ikihitaji sare ya aina yoyote ili kusalia ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja wakati New Power ilikuwa ikihitaji alama tatu kubaki ligi hiyo.

Hivyo, msimu huu kwa Kanda ya Unguja timu ya New Power, Mchangani FC, African Coast na Bridge Star rasmi zimeshuka daraja na zitacheza Ligi Daraja la Mkoa msimu ujao.

# Michezo

Jumatano Juni 22, 2022

Nipashe




'Ninaimani Silva atabaki City'

UKURASA 21

# Simba yaikomalia Yanga kwa Morrison

## ●●● Yawaita mezani huku ikieleza kocha mkuu ataamua endapo...

**Na Saada Akida**

WAKATI kiungo wa Simba, aliyeko mapumzikoni kwao nchini Ghana, Bernard Morrison, akidaiwa kuwa katika orodha ya wachezaji wanaotarajiwa kusajiliwa na Yanga, uongozi wa 'Wekundu wa Msimbazi' hao, umefungua milango yao kwa timu yoyote inayomhitaji kwenda kukaa meza moja ya mazungumzo ya kuvunja mkataba wake.

**Kauli hiyo ya Simba inakuja baada ya tetesi kuzagaa kuwa Yanga wanahitaji kumrejesha kikosini nyota huyo kwa ajili ya kujiimarisha kuelekea msimu ujao wa mashindano yaliyopo mbele yao hususan Ligi ya Mabingwa Afrika na Ligi Kuu Tanzania Bara.**

Zipo taarifa za ndani kabisa kuwa nyota huyo amewaandikia barua uongozi wa Klabu ya Simba, umpe barua ya kuondoka (Release Letter) ili aweze kusajiliwa mapema kuwahi dirisha la usajili la klabu zinazoshiriki michuano hiyo ya CAF.



Simba ambao hawana presha katika suala hilo, wanataka mpaka mkataba wake utamatike kisha wamkabidhi barua nyota huyo ambaye katika barua yake alieleza kuwa kuna klabu ya nje inamhitaji.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally (pichani chini), alisema Morrison ni mchezaji halali wa timu hiyo na mkataba wake unamalizika Agosti mwaka huu na sasa yuko katika mapumziko.

Alisema wako tayari kukutana na viongozi wa klabu au timu yoyote inayomhitaji nyota huyo kwa ajili ya kukaa mezani kuangalia maslahi ya pande zote tatu na kufanya biashara ya kumuuza.

"Morrison bado ni mchezaji wa Simba, mkataba wake utaisha Agosti mwaka huu, kama kuna klabu inamhitaji, ifike mezani kuja kufanya mazungumzo ili tuwauzie," alisema na aliongeza;

"Klabu au timu inayomhitaji Morrison basi ilete ofa kwetu kulingana na thamani ya mkataba wake uliobaki na kama haiwezi, wasubiri hadi Agosti mwaka huu, mkataba wake utakapomalizika," alisema Ahmed.

Alisema baada ya mkataba wa nyota huyo kufikia tamati, itakuwa juu ya kocha wao mpya ambaye atakuja kuchukuwa nafasi ya Pablo Franco.

"Suala la Morrison kubaki ndani ya klabu hii ni la kocha wetu mpya kwa sababu ameanza majukumu yake kwa kukabidhiwa ripoti na sasa anaifanyia kazi na muda wowote tutamtangaza baada ya kukamilisha taratibu za uhamiaji," alisema Ahmed.

ITAKUWAJE...



Morrison.

# Yanga na mkakati mzito CAF

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

HUKU malengo yao sasa yakiwa ni kuhakikisha wanamaliza ligi bila kupoteza, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, amesema kwa sasa wanazingatia zaidi ratiba na Kalenda ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF), hasa katika suala la usajili.

Yanga ambao tayari ni mabingwa wapya wa msimu huu, watashuka Uwanja wa Benjamin Mkapa leo saa 12:30 jioni dhidi ya Polisi Tanzania katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaze alisema licha ya kwenda kucheza mechi dhidi ya Polisi Tanzania kutafuta matokeo, jicho lao lipo kuelekea msimu ujao ikiwamo kutorudia makosa yaliyofanyika msimu uliopita katika michuano ya kimataifa.

Alisema msimu uliopita walianza katika hatua za mzunguko wa kwanza na kutopata matokeo mazuri yaliyochangiwa na kushindwa kutumia baadhi ya wachezaji kwa sababu ya kucheleweshwa kupatikana vibali vya kimataifa (ITC).

"Ni kweli msimu uliopita hatukufanya vizuri jambo ambalo lilichangiwa na kuchelewa kupata vibali, juzi tumepokea barua kutoka CAF, kwamba wamesogeza mbele tarehe badala ya Agosti 12 sasa tunacheza Septemba mwaka huu nina imani tuna muda mrefu wa kukamilisha usajili wetu," alisema na kungeza;

"Tunazingatia sana kuhusu ratiba na Kalenda ya CAF kuhusu michezo ya hatua za mzunguko wa kwanza, tumejifunza makosa ya msimu uliopita kushindwa kutumia baadhi ya wachezaji katika michuano ya kimataifa kwa sababu ya kuchelewa kufika kwa ITC," alisema kocha huyo.

Kuhusu usajili, alisema kwa sasa wanaendelea na tathimini ya mchezaji mmoja mmoja waliocheza msimu huu kuangalia uwezekano wa kuongeza nguvu kwa msimu ujao.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042